

KRISTO AMETAMBULISHWA YEYE

YULE KATIKA VIZAZI VYOTE



Mwaweza kuketi. Hakika ninayahesabu haya kwamba ni majaliwa makuu, kuwa hapa usiku wa leo. Nijuavyo mimi, huu ndio wakati wetu wa kwanza tuliopata kuwa Ta—Tampa kwa ajili ya mkutano. Daima nimetazamia kwa matarajio makubwa ya kuja hapa kuwatembelea. Mahali pa kupendeza sana, na watu wazuri sana ambao...kama tuliokutana nao mtaani. Nasi tuna...Daima nimewazia kungekuwako na mkutano mzuri hapa. Na kwa hiyo tulifahamishwa hivi majuzi kwamba tungekuja hapa, kwa hiyo tumekuwa tukiomba na kungojea fursa hii nzuri sana. Hatimaye imefika.

² Sasa sisi hatuninii, hatutakuwa hapa muda mrefu sana, siku nne tu usiku na Jumapili alasiri. Nasi tunajaribu kuweka kila jitihada tuwezayo, ku—kumwinua Yesu Kristo na kusaidia kuuendeleza Ufalme Wake; tukitumaini ya kwamba tutakapoondoka, kwamba—kwamba kila mmoja atafaidika, kila kanisa linaloshiriki. Na si hilo tu, bali makanisa yote kote nchini yatafaidika na kukaa kwetu.

³ Nami nina hakika tutafaidika kwa kuwatembelea, na kuzungumza nanyi, na kuwahubiria, na kuomba pamoja nanyi. Nasi tuko hapa kuona ni watu wangapi tunaoweza kuwafanya waoko ke katika Ufalme wa Mungu, na halafu pia kuwaombea watu wagonjwa walio wagonjwa na wahitaji.

⁴ Hatujaribu kupachukua mahali pa daktari, sasa, kwa kuwa sisi si daktari. Tu—tunadai tu kumwombea mgonjwa wake, kwamba Mungu atamponya. Na kwa hiyo nina hakika angethamini hilo. Na kwa hiyo sasa ninii ye—yetu. . .

⁵ Tunachojaribu kufanya katika miamsho hii ni kumtukuza Yesu Kristo. Na hilo, nina hakika, halitamwudhi yeyote wenu tunapojaribu kumwinua Yesu Kristo, kwa kuwa hilo ndilo lililotuleta hapa.

⁶ Sasa, kila Mkristo, kila mwaminio ametamani kumwona, kuwa na njia fulani kuwasiliana Naye, na kupata mengi Yake, kumwamini zaidi. Na hilo ndilo lililotuleta hapa kufanya, pamoja, kuona ikiwa hatuwezi kuungana pamoja na kuyaamini Maandiko kwa kusudi hilo.

⁷ Sasa, ndugu zangu hapa, wahudumu, kuwapa mikono, hakika ni—nina furaha kuliona kundi hili la wahudumu wanaoudhamini uamsho huu. Nami siko hapa ku—kuleta chochote kipya, bali ni kushikamanisha tu jarife langu na yao.

⁸ Mwajua, Yesu alisema, “Ufalme wa Mbinguni ni kama mtu aliyechukua jarife akaenda kwenye ziwa, na kulitupa ndani, na, alipolivuta jarife, alikuwa na wa kila namna kwenye jarife hili.”

⁹ Sasa, sisi ni wavua samaki, basi. Na kuna samaki wengi kwenye ziwa hilo, ambao Mungu anawataka. Basi samaki wa mwisho atakapotolewa, yote yamekwisha basi. Sasa hatujui ni lini huyo samaki wa mwisho atakapotolewa humo. Na sasa nipo hapa. . . Jarife moja, tutasema, litafika umbali wa futi *kadhaa* na lingine litafikia futi *kadhaa*. Basi tukiunganisha majarife yetu yote pamoja, nitaunganisha langu na yao, tunaweza kufika mbele kidogo na labda, kwa hiyo, tunaweza kuwashika wengine ambao tusingeweza kuwashika vinginevyo.

¹⁰ Sote tunaamini katika kuja kwa Bwana, kwamba Kuja Kwake kumekaribia. Tunaamini kumekaribia sasa. Hatujui ni wakati gani ambapo Yeye atafika. Kwa sababu hii, tunataka kutoa kila jitihada tujuayo, kuuendeleza Ufalme na kumfanya yule mtu wa mwisho aokolewe katika Ufalme. Basi huyo wa mwisho atakapookoka, hakutakuwako na—hakutakuwako na mmoja zaidi. Itakuwa ni kiasi *fulani* tu. Basi huyo wa mwisho atakapoingizwa, Mwili wa Kristo umekamilika, Unyakuo utatukia.

¹¹ Na kwa hiyo tunaitazamia siku hiyo, tutoke mahali hapa tulipo sasa, kwa kuwa hakika ni—ni nyumba ya wadudu, tunajua hivyo, iliyojaa maradhi, magonjwa, na masikitiko, na taabu. Na, jamani, ni nani angetaka kukaa humu, wakati kuna Mahali bora pa kwenda?

¹² Kwa hiyo tuna—tunajaribu kumfanya kila mtu aokoke, kusudi Yesu apate kuja. Naye hawezi kuja mpaka yule wa mwisho aliye na jina la Kitabu cha Uzima, lililowekwa Mle kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; wakati jina hilo litakapoitwa, hilo ndilo la mwisho basi. Alikuwa kukomboa, kurudisha. *Kukomboa* ni “kurudisha.” Basi atakapomwingiza yule wa mwisho. . . Yeye ameketi mkono wa kuume wa Mungu, usiku wa leo, akifanya kazi Yake ya upatanisho. Basi huyo wa mwisho atakapookoka, ambaye alikombolewa, na kuonekana na kujulikana na Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; wakati mtu huyo wa mwisho atakapookolewa, hiyo inakifunga kile Kitabu. Ndipo Mwana-Kondoo anatokea, anakitwaa kile Kitabu katika mkono wa kuume Wake Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi. Basi ni. . . Yeye yuaja basi, yuaja duniani. Nafikiri kwamba Mungu ni. . .

¹³ Mara nyingi tunashikwa na wasiwasi na tunaanza kuwazia, “Vema, linapaswa kuwa *hivi*, na hatuna budi kulifanya *hivi* ama kulifanya *vile*.” Hatuna chochote cha kufanya katika hilo; tutekeleze tu sehemu yetu ambayo anatuongoza kuitekeleza. Kumbukeni, hakuna kitu kilichoenda kombo.

¹⁴ Yule Mungu mkuu mwenye nguvu zote anajua kikamilifu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kwamba tungeketi hapa usiku wa leo. Kama Yeye hana kikomo, hana budi kujua. Kwa hiyo, asingeweza kuwa asiye na kikomo pasipo kujua mambo yote. Na kwa kujua Kwake kimbele Yeye alijua ya kwamba mkutano huu ungekuwa hapa; na labda ukachaguliwa Naye, ninatumaini kwamba ulichaguliwa, kuwaleta wengine zaidi katika Ufalme Wake.

¹⁵ Mungu, kama hapo mwanzo, Yeye alikuwa tu ni Mungu. Vema, hakuwa ni mungu kweli; alikuwa tu ni wa Milele. Mungu ni... Neno letu la Kiingereza *Mungu* linamaanisha “kitu cha kuabudiwa.” Wala hapakuwapo na kitu cha kumwabudu. Yeye alikuwa akikaa peke yake, Elohimu. Kwa hiyo hapakuwapo na kitu cha kumwabudu, kwa hiyo alikuwa tu ni yule mkuu wa Milele.

¹⁶ Bali ndani Yake mlikuwamo na sifa. Nazo sifa ni mawazo. Kama tu vile inavyokubidi kuwaza jambo lolote kabla hujalinena; ndipo unapolinena, linakuwa ni neno. Halafu Yeye ni wa Milele, na ndani Yake mlikuwamo na sifa. Naye alilineni, Nalo likawa ni Neno, nalo Neno linadhihirishwa. Nalo Neno linapodhihirishwa, ni Mungu akifanyika kitu kinachoonekana.

¹⁷ Na kwa hiyo, kila kitu kiko kwenye wakati wake kabisa, haitubidi kuhangaika juu ya hilo. Yeye, Yeye atakuwa na kila kitu. Kamwe hatamruhusu adui Wake afanye kinyume. Atamwacha adui afanye mambo fulani, kuwaongoza watu kwenye majaribu, kumjaribu mtoto Wa—Wake, na kadhalika. “Kwa kuwa kila mwana amjiaye Mungu hana budi kurudiwa na Mungu, na kujaribiwa.” Kwa hiyo, kama hatuwezi kustahimili marudio, basi tunakuwa watoto haramu wala si vile tunavyodai kuwa.

¹⁸ Kwa hiyo, juma hili, siku zilizosalia katika juma hili, hebu na tuweke imani yetu pale juu kama Uzao wa Ibrahimu kweli, kama tunavyopaswa kuwa. Hebu tumwamini Mungu. Ndipo tutawaombea wagonjwa na kufanya kila tuwezacho, kusaidia safarini. Ndipo tuondokapo, tunatumaini ya kwamba kutakuwako na uamsho wa mtindo wa kale kote humu nchini, hata watu watafurika kutoka kila mahali, wasongamane kwenye makanisa haya, na kadhalika, kwa ajili ya uamsho wa mtindo wa kale.

¹⁹ Ndio kwanza tumalize uamsho mkuu, miaka kumi na mitano, kumi na sita iliyopita. Tumekuwa na mikutano mikuu. Imevunja rekodi zote za historia, kadiri niijuavyo historia. Kwa kawaida uamsho hudumu kwa muda wa yapata miaka mitatu, bali huu umeendelea kwa muda wa miaka mingi. Na sasa mioto ya uamsho inapoa, shauku ya watu inafifia, nanyi mnaweza kuliona. Kwenye li—lile hekalu la kale la Vesta, huko Rumi, wakati mioto ilipopoa, watu walienda nyumbani.

Lakini tunajaribu kuiwasha mioto hii tena juu ya kila kilima tuwezacho. Siwezi kufanya hilo, hakuna mhudumu awezaye; inatuhitaji sisi sote, pamoja, katika maombi, na kumwamini na kumtumaini Mungu, kumwona Roho Mtakatifu akiendelea kuwabariki watu Wake tunapokungojea Kuja Kwake.

²⁰ Sasa, kusudi langu, katika kuwaombea wagonjwa. Nitanena kuhusu hilo sasa: kuwaombea wagonjwa. Ni... Hatujaribu kusema hilo ndilo lililotuleta hapa. Sisi, jambo moja lililotuleta hapa, bali kuwaombea wagonjwa ni jambo dogo. Kamwe huwezi kulifanya kubwa jambo dogo. Tunajua hilo. Kwa hiyo, bali Yesu alikuwa, nafikiri wanakisia yapata asilimia themanini na sita ya huduma Yake ilikuwa ni kuwaombea wagonjwa, kuwaponya wagonjwa. Kwa sababu, katika huo, huwavutia watu.

²¹ Halafu, basi, kila ishara ina sauti nyuma yake. Nayo sauti hiyo haina budi kuwa ni sauti ya Kimaandiko, vile vile hasa inavyopaswa kuwa ni ishara ya Kimaandiko. Halafu ishara hiyo inaambatana na sauti. Kama vile Musa, wakati aliposhuka kwenda Misri; sauti ya ishara ya kwanza, sauti ya ishara ya pili. Na kila kitu kikuu kinachotukia kwa Mungu, kinachotoa ishara, ipo sauti inayoifuata ishara hiyo. Kama vile Yona, wakati alipotolewa kwenye tumbo la nyangumi, hiyo ilikuwa ni ishara; ndipo sauti yake ilikuwa, "Tubuni, la sivyo katika siku arobaini mtaangamia." Kwa hiyo daima kuna sauti inayoambatana na ishara.

²² Sasa, kile tunachotaribu kufanya, ni—ni kujaribu kuwafanya watu kumwamini Bwana Yesu, kumkubali tu, pasipo kuwekewa mikono. Sasa, tunajua kuna Andiko linalosema, "Wekeni mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Nasi hatujaribu kulidunisha Andiko hilo, kwa sababu hilo lilikuwa ndilo agizo Yesu Kristo alilolipa Kanisa, "kuweka mikono juu ya wagonjwa." Lakini, kama mtanivumilia, hiyo ilikuwa zaidi sana ni kama desturi ya Kiyahudi. Sasa, kumbukeni yu—yule msichana aliyekuwa mgonjwa, akafa, bintiye Yairo. Yeye alisema, "Njoo, ukaweke mikono Yako juu ya mtoto wangu, na—naye atapona."

²³ Bali yule akida wa Kirumi, Mmataifa, alisema, "Mimi sistahili Wewe uingie chini ya dari yangu. Sema tu neno, na mtumishi wangu ataishi."

²⁴ Basi Yesu akageuka akasema, "Sijapata kuona imani kama hiyo katika Israeli."

²⁵ Mnaona, njia ya Mmataifa ni kumwamini, kumwamini kabisa. Sasa, tunawawekea wagonjwa mikono, bila shaka, tunawawekea. Lakini tunajaribu ku—kuleta u—uhalisi, kwa Maandiko, wa Yesu Kristo kuwa yupo; ndipo wewe, kwa imani, unaunyosha mkono wako na kumgusa, wewe mwenyewe, unaona, kama yule mwanamke aliyetokwa na damu alivyoligusa vazi Lake.

“Vema,” unasema, “kama angekuwa hapa, ningemgusa.”

²⁶ Biblia inasema, katika Waebrania 3, kwamba, “Yeye sasa ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Yeye anaweza kuguswa vile vile hasa usiku wa leo kama alivyoguswa wakati huo. Kwa hiyo tunataka kumgusa.

²⁷ Kwa kawaida mtu fulani husema, “Vema, unajua Ndugu *Nanii*,” mhudumu fulani, mwinjilisti, “aliniwekea mikono, na, loo, Bwana akaniponya. Wanaweka . . . Ndugu *Nanii* aliniwekea mikono.” Mnaona? Hiyo inamfanya kila mtu atamani kumwona ndugu huyo amwekee mtu fulani mikono. Hata hivyo, si mikono ya ndugu iliyofanya hilo. Ni imani yako, hiyo ndiyo iliyofanya hilo. Kwa hiyo, basi wakati mwinjilisti huyo anapotoka mjini, mchungaji ni jamaa duni tu, mbele ya kusanyiko, kwa kawaida. Mambo fulani yanatukia, uponyaji na kadhalika. Wanafikiri inawabidi kumrudisha mwinjilisti huyo mjini kabla mtu yeyote hajaponywa. Sikilizeni. Kamwe msiamini hilo.

²⁸ Imani yako katika Mungu ndiyo iponyayo. Mnaona? Huna budi kumwamini Mungu. Na sasa kama unaweza kumgusa, basi, haikuwa ni mtu aliyekuwekea mikono. Imani yako ndiyo iliyomgusa, nayo imani yako ikaleta uhalisi. Kwa hiyo basi hakuna mtu aliyekugusa, bali imani yako ilimgusa. Na kwa hiyo hiyo huleta ushuhuda halisi Kwake basi. Hilo ndilo lililotuleta hapa, ku—kumtukua Yeye.

²⁹ Sasa, kila siku, mwanangu atashuka aje hapa na kusambaza kadi za maombi. Kama hayupo hapa, mmoja wa hao wengine, vema, wa uamsho, atazisambaza. Nao huzisambaza kadi za maombi, kadi ndogo tu iliyo na namba juu yake. Usiku baada ya usiku, sisi huziita hizo namba na kuwaombea wagonjwa. Na sasa sisi . . . Na kila siku wanasambaza mpya, kwa sababu watu wanya huja. Na kama wakizisambaza zote, siku ya kwanza, hawapati nafasi kupata kadi za maombi.

³⁰ Halafu basi, katika hilo, hakuna ajuaye mahali hasa ambapo mstari wa maombi utaitiwa, kwa kuwa tumekuwa na ujuzi mwingi wa kuyashughulikia mambo haya. Tulimpata jamaa mmoja, wakati mmoja, akiwauzia watu kadi za maombi, wapate kuja jukwaani, kwa hiyo ilibidi tukomeshe hilo, bila shaka.

³¹ Kwa hiyo basi tunakuja huku, naye mvulana huyo huzileta kadi za maombi mbele zenu, kila alasiri saa kumi na mbili u nusu, naye anazichanganyisha kadi hizi za maombi, papo hapo mbele zenu. Kisha unachukua, nawe huenda ukapata kumi; huyo mwingine akapata thelathini na tano; huyo mwingine tisini; huyo mwingine sitini, namna hiyo. Halafu, tena, yeye asingejua una kadi gani.

³² Na jambo lingine, ndipo ninashuka kuja huku usiku, bila kujua ni wapi hasa tutakapoanzia. Huenda tukaanzia mahali pamoja, mahali pengine, mahali popote, nyuma na mbele. Wakati mwingine ninahesabu ni watu wangapi walio kwenye

safu hii, na kuzidisha na wa safu hii, na kuwagawanya na wa safu hii.

³³ Ilikuwa kwamba, ningemfanya mtoto mdogo asimame na kuhesabu. Na mahali alipokomea, hapo ningeanzia. Amini usiamini, mama alimfanya mtoto asimame moja kwa moja kwenye nambari yake. Tungali—tungali tunashughulika na wanadamu, mnaona, kwa hiyo inakubidi kuninii—inakubidi kulifanya vinginevyo.

³⁴ Kwa hiyo, hii imepangwa sasa, vizuri, kwa miaka mingi, mingi sana. Nasi tutawaombea wagonjwa, kila usiku, Bwana akipenda.

³⁵ Na sasa nawatakeni mniombe. Na, sasa, tunaamini ya kwamba Yesu Kristo angali hai. Tunaamini ya kwamba dini zote huenda zikawa ni sawa; bali hakuna moja yazo na si hata moja yazo iliyo ya kweli ila Ukristo.

³⁶ Mimi ni mmishenari. Nimezunguka ulimwengu mara kadhaa. Nami nimekuwa kwenye kila namna ya huduma za nchi za ng'ambo, na kadhalika, na kuwasikia makafiri, Budha, na—na Waislamu na wengineo, kote, kuizunguka dunia. Bali kuna dini moja tu ya kweli iliyoko kweli, moja ya kweli, iliyo na wokovu ndani yake, na hiyo ni Ukristo.

³⁷ Tuna aina nyingi sana zake, tunazojiita Ukristo, bali kuna Ukristo mmoja. Ukristo sio dhehebu. Si kundi la watu. Ukristo ni Mtu, huyo ni Kristo, na—nanyi ni raia Wa—Wake. Na sasa, tunaamini ya kwamba Yeye yu hai. Alifufuka katika wafu. Tunaamini hayo kwa moyo wetu wote. Nasi tunaamini ya kwamba Yeye yupo papa hapa sasa, tunaamini Yeye yu hai usiku wa leo kama tu alivyowahi kuwa hai. Naye anakuja miongoni mwetu, kujithibitisha Mwenyewe kwamba yupo hapa, kama tu vile alivyokuwa.

³⁸ Tumekuwa, tulikuwa na shule kuu na seminari. Bila shaka, tunapopata hizo, tunaanza kuwapata watu wenye mawazo, nao wanayaingiza. Kama watu wawili walianza, wakubali kuunda—kuunda dhe—dhe—dhehebu, na ingawa ni zuri, hata hivyo, katika kipindi cha mwaka mmoja, kungekuwako na mambo ya kila namna yameingizwa katika dhehebu hilo, maana mnapata mawazo mbalimbali. Na tofa-... Kwa hiyo, ni sawa, linadumisha udugu, wala hamna kitu dhidi yake. Lakini, jambo ni kwamba, huokolewi na shirika lako, na dhehebu lako.

³⁹ Unaokolewa na imani yako binafsi katika Yesu Kristo. Hivyo tu. Kwa hiyo ni kati yako na Kristo, peke yake. Kwa hiyo unayachunguza Maandiko, na kumwamini kwa moyo wako wote, na—na Yeye atakuokoa, ama kukuponya. Kama halitimizi Neno Lake, basi Yeye si Mungu; na kama kweli Yeye hulitimize Neno Lake, inathibitisha Yeye ni Mungu. Mnaona? Kwa hiyo, Yeye, tunamwamini kwa moyo wetu wote.

⁴⁰ Na sasa ninyi ombeni pamoja nami, nasi tutafanya vizuri sana tuwezavyo. Na kila usiku tutajaribu kuwaachilia mapema. Kwa kawaida, huwa tumetoka maskanini ama jengoni kabla ya yapata saa tatu u nusu. Sasa, usiku wa leo huenda ukawa mrefu kidogo zaidi. Sijui kwa hakika. Tungali tuna dakika arobaini na tano, kwa hiyo huenda ikawa kwamba tunaweza kutoka kwa wakati unaofaa, usiku wa leo. Tatazungumza kitambo kidogo.

⁴¹ Lakini, usiku wa leo, ninataka kuweka msingi wa yale tunayotaribu kufanikisha. Na mle ndani, inachukua wakati mwingi zaidi, kuwaelezea, kile hasa tunachokusudia kufanya, kwa utaratibu wa karama kutoka kwa Mungu, kwa Kanisa Lake, kwa watu Wake. Na, hakika, hakika hatuwezi kulifafanua; hakuna njia mwanadamu angaliweza kufanya hilo. Na vipi kuhusu, katika siku tatu au nne usiku, kufanya hivyo. Kwenye wakati tu unapozoea, na hisi zote za kigeni zimeondoka, mkiwa hamfahamiani, vema, basi unaanza kuona watu wengine ambao wamepona. Na mambo yametukia. Umeyachunguza Maandiko, na kusema, “Vema, hilo halina budi kuwa. Sijapata kuliona jinsi hiyo, bali hili hapa.” Nalo halina budi kuendana kutoka Mwanzo hadi Ufunuo.

⁴² Sasa, ninaamini ya kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hayaandikwa katika Biblia hii. Ninaamini anaweza, kwa kuwa Yeye ni Mungu. Lakini mradi tu anafanya kile alichohidi Hapa, ni sawa kwangu. Si—si—siamini kwamba chochote kinapaswa kuongezwa kwenye Kitabu hiki wala kuondolewa Kwake. Ninaamini ya kwamba ni ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo. Ninaamini ya kwamba hivyo ndivyo ilivyo. Na mafundisho yote, kwa vyovyote vile, hayana budi kutoka kwenye Biblia hii.

⁴³ Na endapo mtanipata nikisema mambo na kufanya mambo ambayo si ya Kimaandiko, na Maandiko yaliyoahidiwa kwa ajili ya wakati huu, basi, jambo la kufanya, mnaniwia mimi, kumwona meneja na—na kuhakikisha kwamba nimesahihishwa kwa ajili ya hilo. Kwa sababu, mimi ni mwanadamu, pia. Ninataka kwenda Mbinguni, sawa na ninyi wengine.

⁴⁴ Sasa, usiku wa leo, tutasoma baadhi kutoka kwenye Neno la Mungu la Milele. Na kwanza tutasoma ninii. . . yapata vifungu vitatu kutoka kwenye mlango wa 1 wa Kitabu cha Waebrania, halafu tutasoma kama vifungu vitatu kutoka kwenye mlango wa mwisho, mlango wa 13 wa Kitabu cha Waebrania.

⁴⁵ Sasa, daima sisi husimama tunapotoa heshima, ama kupigia bendera saluti, ama kuimba *Bendera Iliyopambwa Nyota*. Vipi kuhusu Neno la Mungu? Na tusimame tunapolisoma.

⁴⁶ Sasa sikilizeni kwa makini tunaposoma Neno hili la thamani, Waebrania 1. Halafu Waebrania 13, na tuanzie kwenye kifungu cha 5 na kusoma cha 8, vyote pamoja.

Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia mbalimbali,

Mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu.

Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa neno la ahadi yake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketika mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;

47 Sasa Waebrania 13:5.

Msiwe na tabia ya kupenda fedha, mwe radhi na vitu mlivyo navyo, kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.

Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?

Wakumbukeni waliokuwa... wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena kwa kuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni imani yao.

Yesu Kristo ni yeye yule jana, ... leo na hata milele.

48 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa maombi. Na wakati tumeinamishe vichwa vyetu, na mioyo yetu, pia, je! kuna haja hapa, mnetaka zikumbukwe, ambazo mnetaka kusema, kiasi fulani kwa Mungu, wakati mkutano huu unapoendelea, “Mungu, nina haja kubwa. Nikumbuke, Bwana”? Mnetaka ijulikane mnapoinua mikono yenu? Useme, “Nikumbuke. Nipo hapa kwa haja fulani, Bwana.”

49 Baba yetu wa Mbinguni, tunakukaribia, katika Jina hilo lijitoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu, tukijua jambo hili, kwamba Yeye alisema, “Mkiomba Baba lolote katika Jina Langu, mtapewa.” Nasi tuna furaha sana kujua hilo, Bwana, kwamba tuna hakikisho hili, kwamba tunapomba chochote katika Jina Lake, lime—limesikiwa na Mungu. Nasi tunaomba, Baba, usiku wa leo, na ombi langu, mikono yangu yote ikiwa imeinuliwa. Na—nakuomba, Baba wa Mbinguni, ujibu kila moja ya haja hizi. Hapana shaka wapo watu pale ambao wapendwa wao hawajaokoka, na—nao wana maradhi, na—na labda matatizo ya nyumbani, matatizo ya fedha. Na, Ee Mungu, u—ulimwengu huu wa kale hakika ni mgonjwa, kila mahali. Na, sisi, tunakutazamia Kuja Kwako, Bwana, ambapo kutakuwa na miaka elfu moja, mizuri sana, Utawala wa Miaka Elfu, ambamo—ambamo wenye haki watatawala na kumiliki pamoja na Kristo. Tunaitazamia saa hiyo, Bwana. Nasi tunajaribu kuishi namna hiyo, kwamba huu ndio wakati ambapo tunaona kizazi cha mwisho juu ya nchi, nasi tunakungojea Kuja Kwake.

50 Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utaokoa kila nafsi inayoweza kuokolewa, katika nchi hii, wakati mkutano

huu ukiendelea. Tujalie, Baba. Ndipo wakati mkutano huu utakapokwisha, kama tukiwakosa, jalia kutokee uamsho katika makanisa yote.

Na—na hima, Bwana, njoo.

⁵¹ Tunaona matetemeko ya nchi yakiivunja-vunja dunia tena, mahali-mahali, na mioyo ya watu ikivunjika, hofu, mshangao wa mwenyeji, na dhiki, na mataifa. Na sisi—sisi tuko tu mwishoni mwa wakati. Tunawazia juu ya lile tetemeko kuu la nchi hivi majuzi, wala hapajakuwapo na lingine kama hilo; ila, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, kwenye Ijumaa Kuu nyingine, wakati Yesu alipokuwa amekataliwa na ulimwengu, dunia ilitikisika kila mahali. Mungu, Yeye amekataliwa, tena. Dunia ilitikisika, hivi majuzi, na vilima na milima ikadidimia ndani, miji ikaporomoka, na maji yakarushwa hewani, nao ulimwengu mzima ukalihisi. Itakuwaje wakati utakaporudi, Bwana? Si ajabu, “Wanaililia miamba na milima.”

⁵² Hebu na tuwe tayari kwa ajili ya wakati huo mkuu wa kwenda Nyumbani, Baba. Jalia kila haja, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁵³ Sasa, sana sana, ninawatakeni msikilize, mnipe wakati. Na muwe wenye kicho iwezekanavyo, hasa sana wakati tukizungumza. Kwa sababu, msipoyapata maneno hayo, yale tunayopaswa kuzungumzia, kila usiku, basi mtakuja jukwaani bila kujua kile kinachowaleta. Mnaona, hamna budi kuelewa. Mnapaswa kuja kwa ufahamu, na hivyo ndivyo Kristo anavyotutaka tuje. Na endapo...Inakubidi kuwa na imani katika yale unayofanya. Kama huna, kwa namna fulani unaenda ovyoovyo, “Natumaini ndivyo,” kamwe halitatukia. Haliwezi kutukia. Mnaona? Huwezi kuwa na imani kama unaenda hivyo. Inakubidi kujua kabisa kile unachoendea, na kujua kitatendeka. Ndipo, ndipo, wewe, una hakika basi kwamba kitatendeka.

⁵⁴ Sasa, kumbukeni. Msisahau. Somo letu ni, na fungu letu, ni kwamba, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

⁵⁵ Sasa, fungu la somo langu la usiku huu ni: *Kristo Ametambulishwa Yeye Yule Katika Vizazi Vyote*.

⁵⁶ Sasa, Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” nasi tunataka kujua jinsi Yeye angeweza kuwa, jinsi tungemtambua. Kama Yeye yupo hapa kama vile tu alivyokuwa wakati mwingine wowote, basi tungetaka kujua jinsi anavyotambulika miongoni mwetu.

⁵⁷ Kuna watu wengi sana walio na mawazo mbalimbali kumhusu Yeye. Mnaona, kila mmoja, kama mtu binafsi, hujaribu kutoa wazo letu kumhusu Kristo, kile alichokuwa, jinsi anavyoonekana, na—na jinsi wanasaikolojia wameichora picha hiyo. Kama vile, *Kichwa cha Kristo kwenye Miaka Thelathini na*

Mitatu cha Hofmann, na—na Sallman na wengine mbalimbali, bali, mnaona, hatujui hiyo ndiyo iliyokuwa sura Yake. Kwa hiyo kamwe tusingalielewa, ama vile alivyoonekana, na kutiwa rangi tu kwa picha fulani.

58 Kwa hiyo, kama mtu fulani angekuja jukwaani, ama miongoni mwetu, na ana makovu mikononi mwake, na alama za misumari, na alama za miiba kwenye paji la uso wake, na anatokwa na damu, sasa, mnaona, huyo—huyo asingekuwa ni Kristo. Maana, wakati atakapokuja, kila jicho litamwona, na kila goti litapigwa, hapo mwili huo utakaporudi duniani tena. Mnaona?

59 Lakini, yeye angeweza kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele basi? Mnaona? Inatubidi kujua sasa kile—kile alichio.

60 Kama ningewauliza, tuseme, labda Walutheri hapa, ni nini wazo lenu kumhusu? “Mbona,” wangesema, “tu—tunaye kanisani mwetu.” Vema, sitilii hilo shaka. “Lakini Yeye ni *hivi*.” Halafu labda niwageukie Wabaptisti, nao—nao wangukuwa na wazo tofauti kidogo. Nami ningewageukia aina mbalimbali za watu wa full Gospel, kama vile Assemblies of God, Foursquare, Umoja wa Pe—Pentekoste, na—na ma—matawi yake mbalimbali, kila moja huenda ikawa na wazo tofauti kumhusu. Kila mtu binafsi mle ndani huenda akawa ana tofauti. Lakini hao . . .

61 Hatuna budi kuwa na jambo fulani ambapo tunaweza kufikia uamuzi wa mwisho, la sivyo hatutajua mahali—mahali tunapoelekea. Nafikiri kitu ambacho kingetatua hilo ni Neno la Mungu. Na pasipo kujali kanuni zetu za imani na mawazo yetu, Neno la Mungu linapaswa—linapaswa kulitatua.

62 Kwa hiyo, basi, baadhi yao wanadai ya kwamba Yeye—Yeye alikuwa, kwa baadhi ya watu, Yeye alikuwa tu ni m—msimamizi mkuu. “Aliunda ku—kundi la mitume kumi na wawili. Alikuwa msimamizi mkuu.” Tujuavyo sisi, kamwe hakuunda chochote. Kamwe hakufanya kitu kama hicho. Alininii tu . . .

63 Yeye alikuwa ni dhihirisho la Mungu. “Ilikuwa ni Mungu katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Alikuwa akionyesha kile Baba alichokuwa, kwa nafsi Yake. Alisema, “Mimi daima hufanya kile kinachompendeza Baba. Nami na Baba ni mmoja. Baba huishi ndani Yangu. Mnionapo Mimi, mmemwona Baba.” Kwa maneno mengine, Yeye alimdhihirisha Mungu, Roho akiwa ndani Yake kwa wingi sana, hata, “Yeye na Baba, haikuwa kitu cha kushikamana nacho kuwa Mtu yule yule.”

64 Sasa, tunaona hapa ndani, wengine wanawazia, “Yeye alikuwa ni mwanafalsafa.” Alikuwa ni mwanafalsafa. Hakuna shaka juu ya hilo. Yeye . . . Bali alikuwa ni zaidi ya mwanafalsafa.

65 Wengine wao walidhania kwamba ni “nabii.” Yeye, Yeye alikuwa ni nabii. Kweli. Biblia ilisema alikuwa hivyo. Bali alikuwa ni zaidi ya nabii.

66 Baadhi yao walisema, “Yeye alikuwa ni mwalimu. ‘Kamwe mtu hakufundisha namna hii.’” Alikuwa mwalimu, bali alikuwa angali ni zaidi ya mwalimu. Mnaona?

67 Baadhi yao husema, “Alikuwa ni mtu mzuri.” Bali alikuwa ni zaidi ya mtu mzuri. Alikuwa mtu mzuri, lakini alikuwa ni zaidi ya mtu mzuri.

68 Na wakati yote yamejumuishwa, Yeye alikuwa ni Mungu. Kwa hiyo hakuwa chochote pungufu, wala chochote zaidi. Asingeweza kuwa chochote zaidi, hakika. “Lakini Yeye alikuwa—Yeye alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, na kuaminiwa ulimwenguni, na kupokelewa juu utukufuni, kisha akaketi mkono wa kuume wa Baba.”

69 Sasa, tunaona, kupata maelezo Yake halisi, sisi. . . Yohana, katika mlango wa kwanza wa Yohana, alisema, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, na Huyu Neno alikuwa pamoja na Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika Mwili akakaa miongoni mwetu.”

70 Sasa, hapo mwanzo, hapo ndipo wakati ulipoanza, wakati Milele ilipovunjika ikaingia katika wakati. Sasa, baada ya kitambo kidogo, wakati unarudi katika Umilele. Hakika, wakati ni Umilele, pia, bali wakati ni muda uliotengwa. Na hivyo ndivyo, kitu pekee tujuacho, ni inchi, na yadi, na maili, na—na tarakimu, na kadhalika. Bali huo si kitu kwa Mungu. Yeye hana wakati. Yeye—Yeye yupo daima.

71 Yeye ni wa Milele, Naye ndiye chanzo pekee cha Uzima wa Milele kilichopo, umo katika Mungu, Baba yetu. Yeye ni wa Milele, Mwenyewe. Sasa, kwa hiyo, kama tuna Uzima wa Milele, tuna sehemu ya Mungu ndani yetu, na Mungu ndani yetu. Kama sivyo alivyo. . . Basi, hiyo ndiyo njia pekee ungaliweza kuwa na Uzima wa Milele. Sio kitu kilichobuniwa, halafu ukapewa na kanuni fulani za imani, ama ukakiishia, ukalelewa ukawa mwanamume bora zaidi ama mwanamke bora zaidi. Ni Mungu Mwenyewe ndani yako. Kama tu vile ulivyo sehemu ya baba yako hapa duniani; wewe ni sehemu ya Baba yako wa Mbinguni. Na kile ulicho, wewe ni sifa za mawazo aliyokuwazia kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Umedhihirishwa. Ilimbidi kuizalisha, na kadhalika, apate kile ulicho wewe, kukufanya kile ulicho. Ndipo wakati tulipokamilishwa, basi hii hapa. . .

72 Watu wengi sana husafiri kwenye barabara ya maisha, wakichungulia kupitia kioo cha kuangalia nyuma. Zaidi sana, simaanishi kusema hili kuudhi hisi, bali wengi wa wanawake wetu, daima, wanapopita umri wa yapata miaka thelathini, wanataka kurudi na—na kuwa msichana mdogo tena. Na wakifikia hamsini, wangali wanataka jambo lile lile. Si hivyo

tu, bali wanaume, pia. Lakini mtu yeyote anayeangalia kupitia kioo cha kungalia nyuma, atapata ajali ya barabarani, mahali fulani. Huwezi kuendesha barabarani, kote, ukiangalia kupitia kioo cha kuangalia nyuma.

⁷³ Lakini ninaamini yale Paulo aliyosema, “Nikiyasahau yaliyo nyuma, ninakaza mwendo niifikie mede ya wito mkuu katika Kristo.” Mnaona? Usiangalie kile ulichokuwa; angalia kile utakachokuwa.

⁷⁴ Ni—nilikuwa nikiwaoza tena mume na mke wakongwe, wakati mmoja. Walikuwa wametoa nadhiri zao tena. Walikuwa na umri wa miaka themanini na mitatu na themanini na minne, kila mmoja. Nilikuwa nimewapa nadhiri kamili. Nami ni—nikajisikia kiwazimu, nikiwa kijana tu kama nilivyokuwa wakati huo, nikijaribu kuninii. . . Mzee huyo alikuwa amefunga ndoa yapata miaka sitini, yeye na mkewe, nao walikuwa wakitoa nadhiri. Nao walikuwa wanapendana tu kama walivyowahi kuwa.

⁷⁵ Naye alikuwa na ndevu ndefu. Basi nikamwambia... Nikamwambia mke, nikasema, “Unaonaje juu yake?” Vema, nilimwuliza mume kwanza. Nikasema, “Waonaje kulihusu, sababu ya wewe kuwa na ndevu ndefu?”

⁷⁶ Akasema, “Nafikiri mzee wa rika yangu anapaswa kuwa na ndevu ndefu.”

Nikamwambia mke, “Waonaje juu yake?”

Akasema, “Vema,” akasema, “lolote afanyalo John ni sawa kabisa.”

⁷⁷ Kwa hiyo, na—nami nikasema, “Vema, kuna tofauti kubwa kwenu tangu ulipomwoa.”

⁷⁸ Akasema, “Wajua, Bwana amekuwa mwema.” Kasema, “Yeye angali ni mrembo tu kama alivyowahi kuwa.” Kasema, “Unajua, kadiri anavyozidi kuzeeka, ndivyo macho yangu yanaingia giza zaidi.”

⁷⁹ Kwa hiyo ni—niliwazia hilo lilikuwa—hilo lilikuwa ni tamu kwelikweli. Natumaini mke wangu anawazia jambo lile lile. Nami najisikia sote tunajisikia hivyo kulihusu. Kwa hiyo, lakini, wa—walikuwa wamepata maisha. Walikuwa wamepata jinsi ya kuyaishi, mnaona.

⁸⁰ Si kile tusemacho, “Sote tungetaka kurudi,” sisi wazee, “kurudi kwenye umri wa miaka kumi na sita, ama kumi na minane, ishirini, kitu kama hicho.”

⁸¹ Lakini kumbukeni kwamba tulikua na kuishi kuufikia umri huo. Halafu mbona, tukila chakula kile kile, tunakufa sasa, wakati chote kinafanya seli za damu vivyo hivyo? Sayansi haiwezi kulithibitisha. Ni mpango uliowekwa na Mungu. Ulipofikia umri huo, Mungu alisema, “Huo ndio ninaotaka sasa.” Mauti yakauvamia.

⁸² Lakini, unaona, katika ule ufufuo, hakutakuwako na kumbukumbu hata kidogo ya umri wa uzeeni. Tunarudi kwenye ule Umilele, daima. Basi kwa nini uangalie nyuma kwenye huo, kulazimika kukiishia kitu hiki chenye mashaka tena? Vema, angalia moja kwa moja pale, mbele zako kinakaa kiumbe kipya katika Kristo, mwili mpya, ule usiopatikana na mauti ambao hautapita kamwe, kamwe hautazeeka, kamwe hautakuwa na maradhi wala huzuni kubwa. Halafu, angalia, endelea kuangalia mbele yako namna hiyo, kwa ajili ya Kuja Kwake.

⁸³ Sasa, “Hapo mwanzo, Neno, Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Huyo alikuwa ni Yesu Kristo. Yeye alikuwa ni Neno la Mungu.

⁸⁴ Sasa, Mungu atauhukumu ulimwengu siku moja. Tunajua hilo. Na sasa watu wengi hufikiri, wana mawazo yao ya kile atakachouhukumia ulimwengu.

⁸⁵ Sasa kwa marafiki wetu wazuri wa Kikatoliki, kama kukiwapo na yeyote hapa, wanaamini ya kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa Katoliki. Kama akifanya hivyo, ni kanisa Katoliki gani? Mnaona? Maana kuna sura nyingi sana za Ukatoliki. Kuna Katoliki ya Kirumi na Orthodoxi ya Kiyunani, na kadhalika. Mnaona? Vema, kama akiuhukumu kwa ya Kirumi, basi ya Kiyunani imekosea. Akiuhukumu kwa ya Kiyunani, basi ya Kirumi imekosea. Mnaona?

⁸⁶ Kwa hiyo basi kama akiuhukumu kwa la Kilutheri, la Kibaptisti limekosea. Akiuhukumu kwa la Kibaptisti, la Kilutheri limekosea. Akiuhukumu kwa la Kipentekoste, basi yote mawili yamekosea. Basi, mnaona, basi haya basi.

⁸⁷ Yeye hatauhukumu ulimwengu kwa kanisa lolote. Hatauhukumu ulimwengu kwa mfumo wowote wa kanuni wala kanuni yoyote ya imani. Atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo, Naye ni Neno. Yesu ni Neno. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu.” Naye Neno, lingali ni Mungu, “yeye yule jana, leo, na hata milele.” Yeye yule jana, leo, na hata milele!

⁸⁸ Sasa ingewezekanaje? Mungu, hapo mwanzo, aliligawa Neno Lake, kiasi fulani kwa kila wakati. Hiyo ndiyo sababu Yeye alijua mwisho tangu mwanzo. Katika kila wakati kulikuwako na u—unabii uliogawiwa wakati huo. Kwa kawaida, makanisa, na kadhalika, na makundi ya watu, yote yalilipotosha kabisa, mpaka Yeye angemtuma nabii jukwaani. Sasa, tunajua Biblia ilisema, kwamba, “Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi, na kwa njia mbalimbali, siku hizi za mwisho amesema na sisi katika Mwanawe, Yesu Kristo.” Kamwe, Mungu asiyebadilika kamwe habadilishi njia Yake ya kufanya mambo. Mungu anayo njia moja ya kufanya mambo, Naye habadiliki, kamwe.

⁸⁹ Wakati mwanadamu alipotenda dhambi akaanguka, katika bustani ya Edeni, Naye Mungu akafanya njia kwa mtu huyo ku—kuokolewa, Yeye kamwe habadilisha njia Yake. Yeye alimkubali mtu huyo juu ya msingi wa Damu iliyomwagika ya Yeye asiye na hatia, wala kamwe hajaibadilisha, tangu, haidhuru nini.

⁹⁰ Tumejaribu kujenga minara, Nimrodi. Na tunajaribu kuninii... Tunajaribu kujenga miji, kama Nebkadreza. Tumejaribu kuwa na madhehebu, kuwaingiza watu wote kwenye kundi moja. Tumejaribu kuwaelimisha waingie kwake. Tumejaribu kila kitu ulimwenguni, kufanya hivyo. Nayo, kila kitu, kimeshindwa.

⁹¹ Mungu hukutana na mwanadamu kwenye msingi mmoja, huo ni chini ya Damu iliyomwagika, na hapo ndipo mahali pekee atakapopata kukutana naye. Nje ya hapo, unafanya kazi bure. Yeye alikutana na Israeli, alikutana na Ayubu, alikutana na manabii wote, kila mahali, chini ya damu iliyomwagika. Na hivyo ndivyo tu atakavyokutana nasi, usiku wa leo; sio kama Wapentekoste, sio kama Methodisti, sio kama Lutheri, sio kama Katoliki. Bali atakutana nasi chini ya Damu iliyomwagika ya Mwanawe, Yesu Kristo, na hiyo peke yake. Hapo ndipo mahali pekee atakapokutana nasi.

⁹² Mungu asiyebadilika, Yeye kamwe habadilishi njia Yake ya kufanya chochote. Mnaona? Tabia Yake inathibitisha ya kwamba Yeye habadiliki, Mwenyewe.

⁹³ Yeye kamwe hajishughulishi na makundi. Baadhi yake, makubwa, mnasema, “Dhehebu letu kubwa.” Mungu hatajali hilo. Yeye hushughulikia mtu binafsi, mtu mmoja. Mnaona?

⁹⁴ Maana, wewe ni mtu binafsi tu, wewe mwenyewe. Hamna pua mbili zinazofanana, hamna alama mbili za vidole gumba. Wewe ni mtu binafsi, Naye Mungu hukushughulikia kama mtu binafsi.

⁹⁵ Kwa hiyo, katika kila wakati, wakati Mungu anapoligawa Neno Lake kwa ajili ya kila wakati, basi, wakati Neno hilo liko tayari kudhihirishwa. Sasa yachunguzeni Maandiko; msilichukue tu neno langu. Wakati Neno hilo linapokuwa tayari kudhihirishwa, basi Mungu anamtuma nabii na kulifunua Neno kwa nabii Wake. Biblia ilisema, “Neno la Bwana liliwajia manabii. Wala Yeye hafanyi neno lolote bila kuwafunulia manabii Wake.” Nabii ndiye ambaye... ambapo Neno la Bwana huja, kama vile ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na siku za—za Eliya, na siku za—za Musa, na kadhalika. Yeremia, na Isaya, na ni nani mwingine ningaliweza kusema, kwamba, Yeye aliwajia hao. Nao wakadhihirisha, ama kulitimiza, hilo Neno.

⁹⁶ Sasa, angalieni, kusudi mpate kuona kama tuko sahihi, au la, katika mawazo haya tunayowazia.

⁹⁷ Sasa, mnaona, kila mmoja wetu angekuwa na mambo, kila mmoja wetu huifasiri Biblia tofauti. Mmethodisti anasema, “Linapaswa kusomwa namna *hii*.” Mkatoliki anasema, “Namna *hii*.” Lutheri, “Namna *hii*.” Wapentekoste, “Namna *hii*.”

⁹⁸ Bali Biblia inasema, kwamba, “Neno la Mungu si la kufasiriwa apendavyo mtu yeyote.”

⁹⁹ Mungu hulifasiri Neno Lake Mwenyewe. Mungu hahitaji mfasiri yeyote. Hatuhitaji kufasiri. Mungu anapotoa ahadi na kuidhihirisha, na kuitimiza, hiyo ndiyo tafsiri yake. Mungu alisema, hapo mwanzo, “Iwe nuru,” ikawa nuru. Hilo halihitaji tafsiri yoyote. Mungu aliposema, “Itakuwa nuru,” mara nuru ikawa, hilo linafasiri Neno Lake Mwenyewe. Alisema, “Bikira atachukua mimba,” naye akachukua. Alisema “angeimwaga Roho Yake katika siku za mwisho, juu ya wote wenye mwili,” Naye akaimwaga. Halihitaji fasiri yoyote. Mungu anapolifanya Neno Lake dhahiri kwako, huko ni kutoa fasiri Yake.

¹⁰⁰ Sasa, Musa alipokuja, asingeweza kuuchukua ujumbe wa Nuhu. Wala Musa asingalichukua...ama—ama Nuhu kuuchukua ujumbe wa Musa. Wala Yoshua asingaliweza kuuchukua ujumbe wowote wao, mnaona, kila mmoja. Isaya asingeweza kuchukua wa mwingine. Kila ujumbe ni kwa ajili ya wakati huo.

¹⁰¹ Na pamoja na wakati tunaoishi, Neno hilo linapofasiriwa, Mungu akinena Neno hilo na kulifanya hai Neno la wakati huo, akitoa tafsiri yake, huyo ni Mungu katika Kristo, akidhihirisha. Mnaona? Kwa kuwa, Kristo ni Neno, na wakati Neno linapodhihirishwa, huyo ni Kristo katika kila wakati, basi.

¹⁰² Mungu Ndiye aliyekuwa katika Yusufu. Tabia ya Yusufu ilimfananisha na Kristo kabisa. Yeye alizaliwa katika wakati wa lile kanisa kuu pale pamoja na baba yake. Ndugu zake walimchukia kwa kuwa alikuwa ni wa kiroho. Aliona maono na angeweza kufasiri ndoto, nao ndugu zake wakamchukia, bila sababu. Kama hiyo siyo sababu hasa ya wao kumchukia Yesu!

¹⁰³ Pia angalieni, alipendwa na baba yake; vivyo hivyo Yesu. Akauzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha; kama Yesu. Akatupwa kwenye handaki, na kudhaniwa amekufa; kama tu Yesu. Akachukuliwa na kuwekwa gerezeni; kama tu Yesu, msalabani. Kisha akatumwa kwa nyumba ya Farao, akawa mkono wa kuume wa Farao; na kama tu Yesu, alivyopaa juu kwenye mkono wa kuume wa Mungu. Na wakati Yusufu alipoondoka kwenye ikulu, parapanda zililia, na kila goti ilibidi lipigwe, Yusufu alikuwa yuaja; na kwa hiyo Yesu atakapoondoka kwenye Kiti cha Enzi, na kurudi, baragumu italia, na kila goti litapigwa.

¹⁰⁴ Yeye alikuwa ndani ya—Yeye alikuwa ndani ya Daudi. Wakati Daudi alipokataliwa na watu wake mwenyewe, kuwa mfalme, na kupanda juu ya kilima, akaangalia nyuma juu ya

Mlima wa Mizeituni; wakati alipokuwa akifukuzwa kutoka kwa watu wake mwenyewe, alipanda kilima, akaangalia nyuma juu ya ule mji, kisha akalia. Miaka mia nane tangu hapo, Mwana wa Daudi aliketi kwenye kilima kile kile, akilia, kwa kuwa alikuwa amekataliwa katika mji Wake Mwenyewe. Ndipo kasema, “Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi ningaliwafunika kama vile kuku awafunikavyo vifaranga wake, bali hamkutaka.” Mnaona? Ni Kristo katika kila kizazi. Huyu alikuwa ni Kristo katika Daudi.

¹⁰⁵ Biblia ilisema, “Musa aliacha hazina za Misri, anasa na utajiri wa Misri, akahesabu kuwa shutuma ya Kristo ni hazina kuu.” Naye akamfuata Kristo nyikani, ambaye alikuwa ni Nguzo ya Moto. Hiyo, vema, ilikuwa ni Logos iliyotoka kwa Mungu, ambayo ilikuwa ni Kristo, aliyetiwa mafuta.

¹⁰⁶ Na sasa, tunaona ya kwamba katika kila moja ya nyakati hizo, kwa kawaida watu hawataki kuamini, kwa sababu tayari wana mwelekeo wao. Unapiga kona. Unajenga jengo. Kisha unafika kwenye kona, kila mtu anakimbia *huku*, hawataki kupiga kona hiyo. Lakini jengo linaelekea kule, kama Neno linasema linaelekea kule. Mnaona? Hapo ndipo tunapopata hizo njia panda za wakati. Hapo ndipo pagumu. Hapo ndipo watu hutokwa na jasho.

¹⁰⁷ Sasa, kumbukeni, Mungu kamwe habadilishi njia Yake ya kufanya mambo; daima kote katika Maandiko, vivyo hivyo tu. Sasa, katika siku za Nuhu, huyo aliyekuwa katika Nuhu alikuwa ni Kristo. Huyu alikuwa ni Nuhu. . .

¹⁰⁸ Ilikuwa ni Kristo ndani ya Musa. Angalieni, alizaliwa kwenye wakati, alizaliwa kuwa nabii, naye akawekwa kwenye manyasi; na kama vile tu ilibidi Kristo aondolewe nchini, sababu ya mauaji ya watoto wote. Ndipo alipokuja huko nyikani, mtoa sheria, na—na kuhani, na na—na—nabii, na kadhalika, kila kitu kilimwonyesha Kristo kimbele, kabisa, kote kote kupitia kwa manabii kama walivyotabiri.

¹⁰⁹ Sasa tunaona Yeye, Mungu, basi akijitambulisha Mwenyewe katika nyakati zote. Jinsi gani? Yeye alijitambulishaje sasa? Alitumia tabia gani? Tabia Zake zile zile, tangu mwanzo: akilidhihirisha Neno Lake, akilifanya Neno Lake kuishi. Huo ndio utambulisho, Neno lililoahidiwa la wakati huo. Mnaona?

¹¹⁰ Sasa, wakati Musa alipokuja, yeye asingalisema, “Sasa tutajenga safina na kuelea kutoka hapa.” Huo ulikuwa ujumbe wa Nuhu. Na hiyo ndiyo shida. Wakati Yesu alipojitokeza jukwaani, aliwakuta hao Waebrania wakiishi katika mng’ao mkuu wa nuru nyingine. Na hivyo ndivyo ilivyo leo hii. Hivyo ndivyo ilivyo katika kila wakati. Wanaishi katika mng’ao wa nuru nyingine.

¹¹¹ Hiyo ndiyo sababu ninyi Wamethodisti, mlipojitokeza jukwaani, Luther alikuwa. . . Mlikuwa mkiishi, na mlikuwa

mkiishi katika mng'ao mkuu wa wakati wa Kilutheri; wasingeweza kumkubali John Wesley. Wakati Pentekoste ilipokuja, Wamethodisti wasingeikubali Pentekoste, kwa kuwa walikuwa wakiishi katika mng'ao mkuu wa Methodisti. Na sasa sijui Wapentekoste wanaishi katika mng'ao wa aina gani? Mnaona?

¹¹² Jambo unalopaswa kufanya ni kuyachunguza Maandiko uone ile saa tunayoishi, halafu ni kitu gani kinachopaswa kuwa hapa wakati huo, na uone kama Mungu analifanya hilo hai na kulidhihirisha, basi hilo ndilo jambo tume—tumepata ufasiri wa kweli kwa wakati huo.

Sasa Yesu, wakati alipokuja, wao walisema, “Tunaye Musa.”

¹¹³ Akasema, “Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi. Yeye aliandika habari Zangu.” Akasema, “Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani yake mnafikiri mna Uzima wa Milele; Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Kwa maneno mengine, “Angalieni katika Maandiko.” Mnaona?

¹¹⁴ Loo, walikuwa wameshika mapokeo yao sana. Yeye alisema, “Naam, kwa mapokeo yenu, mmelitangua Neno la Mungu kwa watu. Mmewaweka katika mapokeo sana, hata Neno halina nguvu juu yao. Kwa kuwa mnasema . . .”

Ni jambo lile lile sasa. “Mimi ni *hili*. Mimi ni mfuasi wa *hili*.”

¹¹⁵ Nilimwuliza msichana, wakati mmoja, “Je! wewe ni Mkristo?” Akasema, “Mimi huwasha mshumaa kila usiku.” Sasa, kana kwamba hilo lilikuwa na uhusiano wowote Nalo.

¹¹⁶ Nilienda kuomba hospitalini, wakati mmoja, kumwombea mama fulani. Akasema, “Ngoja. Vuta hayo mapazia. Vuta hayo mapazia.”

Nikasema, “Kuna nini?”

Akasema, “Sisi ni Methodisti.”

Nikasema, “Kwani wewe si Mkristo?”

Kasema, “Mimi ni Mmethodisti.”

¹¹⁷ Nikasema, “Vema, hivyo tu. Hilo latosha, basi. Wewe si Mkristo. Wewe ni Mmethodisti tu.”

¹¹⁸ Kwa hiyo basi, jambo ndilo—ndilo hilo, mnaona, kamwe hawalipati hilo. Na, mnaona, wanaishi katika mng'ao wa nuru nyingine. Nao mng'ao ndicho kitu . . . Ni kitu gani? Ni nuru ya bandia. Ni uakisi. Kama mimi . . .

¹¹⁹ Nyumba yangu iko Tucson, Arizona. Ninaishi jangwani. Mna mazigazi. Mnajua ni kitu gani. Hayo ni uakisi wa jua kwenye jangwa lenye joto, nalo linaakisi nuru ya bandia, inaifanya ione kane kama ni maji. Unapofika hapo, hapana maji hapo.

¹²⁰ Huo ndio mng'ao. Na ni kitu kinachokupa matumaini, wala hukipati.

¹²¹ Na, sasa, wizi mkubwa kuliko wote uliopata kufanywa ulimwenguni, ulikuwa ni ule wa dola milioni saba ambao ndio kwanza ufanywe Uingereza. Ulifanywa kwa taa bandia. Waliweka taa kule nje na kulifanya garimoshi lipunguze mwendo, wala hata Scotland Yard isingeweza kuzipata. Ndio wizi mkubwa kuliko wote uliopata kutokea katika historia ya ulimwengu, ulifanywa kwa nuru bandia.

¹²² Nao wizi mkubwa kuliko wote uliopata kutokea katika kanisa la Yesu Kristo, ni nuru bandia, mng'ao wa wakati mwingine, wakati Mungu anapojaribu kuingiza, ama kuonyesha, kwa watu, Nuru ya wakati huu.

¹²³ Yesu alipokuja, Yeye alikuwa ni Neno. Vivyo hivyo Musa alikuwa ni Neno; Musa, hao manabii wengine, walikuwa ni Neno, bali walikuwa Neno katika sehemu. Yeye alikuwa Neno katika utimilifu. Alikuwa ni utimilifu wa Neno. Yeye alikuwa ni Neno.

¹²⁴ Halafu walikuwa wakiishi katika m—mnga'o unaometameta wa wakati wa Musa. Yeye akasema, "Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi, kwa kuwa Musa aliandika habari Zangu."

¹²⁵ Wakasema, "Vema, Wewe hujafikisha bado umri wa miaka hamsini, na wasema 'Umemwona Ibrahimu?' Sasa tunajua Wewe una wazimu."

Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO."

¹²⁶ Yule "MIMI NIKO" aliyekuwa kwenye kichaka kilichowaka moto. Hiyo ilikuwa ni ile Nguzo ya Moto. Mnaona? Yeye alikuwa "MIMI NIKO." "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," Biblia ilisema, "Yesu Kristo." Tabia Zake hazibadiliki, hata kidogo. Maneno Yake ni yale yale.

¹²⁷ Ni sehemu ya Neno kwa ajili ya kila wakati. Naye analifanya lijulikane kwa njia gani? Yeye hulifanya lijulikane kwa watumishi Wake, manabii. Yeye ninii yote. . . Nabii ana—anafahamikaje? Anapotabiri lolote, nalo linatimia.

¹²⁸ Sasa, manabii sasa, katika siku hizi, tuna karama za manabii. . . karama za unabii, hasa. Unawekea mikono, na kuomba, nawe. . . Karama zinaingia, katika karama tisa za roho, kanisani. Hiyo ni, kabla unabii haujapokelewa na kanisa, hauna budi kuamuliwa na waamuzi watano wa kiroho. . . ama waamuzi watatu wa kiroho.

¹²⁹ Lakini, sio nabii. Nabii anazaliwa akiwa nabii. "Karama na miito havina majuto." Ni kitu ambacho kimo ndani yako. Ni kitu ulichozaliwa nacho. Mungu alikichagua ndani yako.

Mbona, Musa alizaliwa akiwa nabii.

¹³⁰ Yeremia, Biblia ilisema, mbona, alisema. . . Mungu alimwambia Yeremia, kasema, "Kabla hata hujaumbika katika tumbo la mama yako, nilikutakasa na kukuchagua kuwa nabii kwa mataifa."

¹³¹ Yohana Mbatizaji, miaka mia saba na kumi na mbili kabla hajazaliwa, Isaya alimwona, “Sauti ya mtu aliaye nyikani.” Baba yake alikuwa kuhani. Yeye. . . Ni, kwa kawaida, wanarudi na kuchukua kazi ya baba yao. Lakini kazi yake ilikuwa muhimu sana. Ilimbidi kumtangaza Masihi. Kwa hiyo akaenda nyikani. Hamna elimu; hakuhitaji elimu. Ilimbidi apate ufunuo wa moja kwa moja, kwamba Masihi huyu alikuwa ni Nani.

¹³² Naye alimjua. Akasema, “Ninashuhudia, nilimwona Roho wa Mungu, kama hua, akishuka juu Yake, ndipo sauti ikatoka Mbinguni, ikisema, ‘Huyu ni Mwanangu Mpendwa.’ Huyu Ndiye.”

¹³³ Kama angalikuwa katika seminari fulani, ama kitu fulani, walisema, “Sasa, mnajua Ndugu Jones, hapa. Yeye anaonekana tu kama Masihi,” mnaona, washawishike.

¹³⁴ Lakini, kazi yake ilikuwa muhimu mno. Ilimbidi kuingia nyikani na kukaa peke yake pamoja na Mungu. Wakati alipotoka, hakuwa na elimu. Alizungumza kama wanadamu. Akasema, “Loo, enyi uzao wa nyoka, ama nyoka kwenye nyasi.”

¹³⁵ Sasa kama ingalikuwa ni mtu fulani mwenye elimu, angalisema neno lingine, mnajua, “Enyi maskini kipande cha usumbufu,” ama kitu fulani. Lakini alikuwa ameleta kitu fulani, bali angali—angalileta neno lingine gumu, la kimaadili ama kitu kama hicho, elimu yake.

¹³⁶ Bali Yohana alisema, “Walikuwa wanyemelezi na telezi kama nyoka.” Hao ndio aliowaona huko nyikani. Kasema, “Enyi uzao wa nyoka, ni nani aliyewaonya kuitoroka hasira ijayo? Msiwazie kwamba, ‘Sisi ni wafuasi wa *hili*, na ni wafuasi wa *lile*,’ mna chochote.” Unashangaa kama asingesema jambo lilo hilo leo hii? “Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto, mawe haya.” Kile alichokuwa ameona. Pia, “Shoka limewekwa kwenye shina la mti.” Kile alichokuwa ameona nyikani. “Kila mti usiozaa matunda mazuri, miti ya matunda isiyozaa, ilikatwa na kutupwa motoni.” Mnaona? Mahubiri yake yalikuwa katika mifano. Bali a—alikuwa vile hasa Mungu alivyomchagua kuwa. Mnaona? Yeye alikuwa ndiye yule nabii. Hawakuwa wamepata nabii kwa mamia ya miaka. Angalieni, bali Mungu alimfinyanga na kumfanya.

Tunaona, Yeremia, akija jukwaani.

¹³⁷ Tunaona, manabii mbalimbali wakijitokeza jukwaani, ni vigumu sisi kujua wanakotoka. Waliinuka tu kisha wakaondoka. Mungu aliwatumia, akawatia muhuri, akawatuma, na ni hivyo tu. Ujumbe ukaendelea. Neno likathibitishwa. Na hilo likaenda kwenye kizazi kingine, ndipo wakajenga juu ya yale manabii hawa waliyofanya. Nao. . .

¹³⁸ Ndipo alipokuja, Yesu alisema, “Mmepaka kuta chokaa, na ma—makaburi ya manabii, nanyi ndinyi mliowaweka mle.” Mnaona?

¹³⁹ Mtu atainuka na ujumbe, na kuuhubiri ujumbe huu, na kutoa ujumbe wa wakati, halafu baada ya kitambo kidogo anauawa, na kuwekwa kaburini. Basi miaka kadhaa baadaye, wanaunda dhehebu juu ha *hili*, na juu ya *hilo* mnatokea kitu kingine. Mnafanya nini? Ujumbe wa mtu huyo tayari umepita. Ni historia. Tunasonga mbele, tukiangalia mbele.

¹⁴⁰ Sayansi haiangalii nyuma na kusema vile sayansi fulani inavyosema. Nilisoma ambapo sayansi ilithibitisha, kwa kuufingirisha mpira; na—na—na huko Ufaransa, yapata miaka mia tatu iliyopita, “Kama mtu akipata kwenda kwa mwendo wa kasi sana wa maili thelathini na tano kwa saa, angeondoka duniani.” Nami nilishuka kuja huku kwa yapata maili sitini kwa saa. Mnaona? Kwa hiyo sayansi hairejei nyuma kwa hilo. Wanaendelea kupiga hatua. Wamemfanya sasa kwenda mamia ya maili kwa saa. Na ninii tu...Hawasimami hapo. Wanaendelea tu kusonga mbele.

¹⁴¹ Lakini, sisi, tunaangalia nyuma kuona kile, “Finney alisema nini? Sankey alisema nini? Moody alisema nini?” Walikuwa ni watu wazuri; vivyo hivyo na Musa na Yusufu. Na huo ulikuwa ni wakati mwingine.

¹⁴² Hebu tuone kile Neno lisemacho, leo, alichu Yesu Kristo. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na njia pekee tutakayopata kujua kile alichu leo hii, ni kuona kile alichokuwa jana, ndipo mtaona kile alichu.

¹⁴³ Sasa, hatuna wakati wa kuweka mengi mno ya hayo, usiku huu, kwa maana tuna dakika chache tu zilizosalia. Angalieni. Neno lililokusudiwa kwa ajili ya kila wakati, wakati Neno hilo linapodhihirishwa, hilo ni Kristo wa siku hiyo, kama vile tu ilivyokuwa katika kila moja ya siku hizo.

¹⁴⁴ Sasa, tunapomwona Yesu akijitokeza ju—jukwaani, Yeye alikataliwa, hata hivyo, alikuwa ni Neno lililoahidiwa. Sasa, katika Kumbukumbu la Torati 18:15, Musa alisema, “Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii kama nilivyo mimi. Na itakuwa ya kwamba kila asiyemsikia Nabii huyu, ataondolewa miongoni mwa watu.” Sasa Huyu hapo, Nabii hasa wa wakati huo, na walimu wa siku hiyo hawakuliona. Hatimaye walimwua. Mnaona? Naye alifanya vile vile hasa.

¹⁴⁵ Yeye alizaliwa na bikira. Hawakuamini hilo. “Hilo lilikuwa ni lundo la ulokole.” Bali tunaliamini sasa, likiisha kuthibitishwa.

¹⁴⁶ Joan wa Arc, wakati alipojitokeza jukwaani huko nyuma katika Ufaransa, yale Mapinduzi ya Kifaransa, ninyi Wakatoliki mlifanya nini? Mlimwua, ati ni mchawi, kwa sababu aliona maono, akafasiri ndoto. Miaka mia mbili baadaye, mlifanya vitubio, mkaichimbua miili ya hao makasisi, waliowaua na kumchoma kwenye nguzo, kisha mkawatupa mtoni. Hivyo ndivyo vitubio vyenu. Mnaona?

¹⁴⁷ Kamwe hamkumjua Mtakatifu Patrick wakati alipokuwa duniani, ambaye aliitwa Sucat. Kamwe hamkumjua. Mnadai kwamba ni mmoja wa watakatifu; angalieni maelfu mangapi ya watoto wake mliowaua huko Ayalandi. Mnaona?

¹⁴⁸ Ni baada ya yote kwisha, uthibitishaji wake umekwisha, ndipo wanaujengea kaburi. Ujumbe umepita tayari na unaingia katika kitu kingine. Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa ajili ya yale Yeye amefanya, akitazamia yale atakayofanya, na kupuuza yale anayofanya. Hivyo ndivyo ibilisi anavyowataka wawe, wasomi na walimu wa kidini sana: wanathibitisha yale aliyofanya, na kuthibitisha yale atakayofanya, huku wakipuuza yale anayofanya. Mnaona? Hapo ndipo imekuwa daima, vile vile. Tungeweza kuendelea na kuendelea mbele, kupitia hayo.

¹⁴⁹ Lakini hebu turudi nyuma kwa dakika chache tu sasa na kutambulisha kile Yesu alichokuwa alipokuwa humu duniani. Nasi tutaona kile alichokuwa wakati huo, kile amekuwa katika nyakati zingine, ndipo itabidi iwe ni kitu kile kile katika wakati huu, kulifanya sawa. Sasa tunaona, wakati alijitokeza jukwaani, hatuna . . .

¹⁵⁰ Tunajua Yeye alikuwa ni Neno. Alikuwa ni Neno. Nalo Neno daima husahihisha kosa. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁵¹ Kwa ajili ya wazo dogo tu hapa, angalieni kwenye . . . ninyi watu mnaomwabudu Mariamu. Mnaona? Yeye alisema Roho Mtakatifu alimtia uvuli ndipo akamzaa huyu Mwana, na, “Alikuwa ni wa Roho Mtakatifu.”

¹⁵² Basi alipokuwa na umri wa yapata miaka kumi na miwili, walikuwa huko Yerusalemu, kwenye sikukuu ya Pasaka, na wakati waliponinii . . . ama Pentekoste. Ndipo wakati waliposhuka kurudi, ilikuwa ni safari ya siku tatu, walikuwa wamemkosa. Kwa hiyo wakarudi kumtafuta, Naye huyo hapo kwenye jumba hilo la mikutano kule, kanisa, akihojiana tu na hao makuhani na kadhalika. Na kwa hiyo mama yake akaenda kule, yeye na Yusufu. Naye akasema, “Mimi na baba yako tumekutafuta kwa machozi.” Mnaona? Mbele ya hao makuhani, aliukanusha ushuhuda wake mwenyewe, akimwita Yusufu baba Yake. Mnaona? Yeye alisema kwamba “Mungu” alikuwa Ndiye Baba Yake, naye hapa akasema, “Mimi na baba yako tumetafuta kwa machozi.”

¹⁵³ Angalieni hilo Neno. Huyo mvulana mwenye umri wa miaka kumi na miwili, hakika, labda hajaingia shuleni hata siku moja maishani mwake. Liangalieni hilo Neno, hata hivyo. Yeye alikuwa ni Neno. Akasema, “Hamjui kwamba inanipasa kuwa kwenye shughuli za Baba Yangu?” Kama Yusufu angalikuwa ndiye baba Yake, angalikuwa pamoja naye kule chini kwenye duka la seremala. Lakini Baba Yake alikuwa ni Mungu, Naye alikuwa akiwanyosha hao makuhani. Huyo, na

hapo angekuwa “kwenye shughuli za Baba Yangu.” Angalieni Neno likilisahihisha kosa. Daima husahihisha, kila wakati. Yeye hakuninii, labda hakuliona, naye akaendelea, akipapasa-papasa. Watu hufanya jambo lilo hilo siku hizi.

¹⁵⁴ Lakini Mungu na atuhishe sasa, kwa dakika hizi zingine chache, tuone kile alichokuwa.

¹⁵⁵ Sasa tunaona, tangu ubatizo Wake, kuingia nyikani, kisha akatoka nyikani.

¹⁵⁶ Basi kulikuwako na jamaa fulani, jina lake Andrea, alikuwa akihudhuria mikutano ya Yohana. Wala asingeweza kumpata ndugu yake, Simoni, kwe—kwenda mikutanoni. Hatimaye, siku moja, walipokuwa wakiosha majarife yao, a—alifika mahali ambapo a—alikutana na Yesu. Naye Simoni alijua, moyoni mwake...

¹⁵⁷ Nilisoma hadithi ndogo juu yake, hapa si muda mrefu uliopita, juu ya Simoni. Baba yake, Yona, ni mwaminio hodari, ni Farisayo. Alisema ya kwamba, “Mara nyingi... Mwanangu, ninazeeka na kuingia mvi.” Akasema, “Ni—niliomba mara nyingi sana kwamba Mungu a—anijalie nimwone Masihi.” Kisha kasema, “Tulimtumainia Mungu kwa ajili ya samaki wetu, tupate riziki. Na—naye mama yenu ametuacha sasa, na inaonekana kana kwamba sitaweza kumwona. Ni—ninazeeka mno.” Kisha kasema, “Sasa, mwanangu, ninataka uketi hapa karibu nami. Ninataka kukwambia.

¹⁵⁸ “Sasa, kabla tu ya Masihi huyo kutokea, kutakuwako na kila namna ya mambo ya uongo yakiendelea. Huyo ni Shetani.” Akasema, “Lakini kumbuka, utamtambua tu Masihi, daima dumu na Neno. Musa alisema, ‘Bwana Mungu wetu atatuondokeshea Nabii.’ Sasa, hatujakuwa na mmoja kwa mamia ya miaka. Lakini atatokea Nabii, Nabii aliyetambulishwa atainuka miongoni mwa watu, huyo atakuwa ni Masihi. Ndiye atakayefuata.”

¹⁵⁹ Ndipo wakati Andrea alipompeleka huko kumwona Yesu, na akamwambia kuhusu Yohana kuhubiri, na kusema Masihi alikuwa yuaja, kwake ilikuwa, vema, jamaa mwingine tu mpita njia.

¹⁶⁰ Kwa hiyo, siku moja, Simoni alikuja moja kwa moja katika Uwepo wa Bwana Yesu Mwenyewe. Ndipo Yesu akamwangualia na kusema—akamwangualia na kusema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Hilo lilitosha. Mnaona?

¹⁶¹ Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba hiyo ni sifa ya Neno la Mungu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. Sasa, Waebrania, mlango wa 4, kifungu cha 12 ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga wenye makali kuwili, na huyatambua mawazo yaliyo moyoni.” Hivyo ndivyo hao manabii walivyokuwa. Hao, hapo ndipo walipoona mambo kimbele, mnaona, na ilikuwa ni kweli kabisa, kwa kuwa lilikuwa ni Neno

la wakati huo. Kama unaelewa hilo, inua tu mkono wako, kimya. Kwa hiyo, mnaona, lilikuwa ni Neno la wakati huo. Hilo ndilo lililowatambulisha hao kuwa nabii.

¹⁶² Sasa, nabii, neno le—letu la Kiingereza *nabii*, linamaanisha “mhubiri.”

¹⁶³ Lakini katika Agano la Kale, hakuwa ni nabii hasa, alikuwa ni mwonaji. Naye mwonaji alitabiri mambo ambayo yangetimia. Na, pia, hizo zilikuwa ndizo sifa zake kama mfasiri wa kiungu wa Neno lililoandikwa, kwa sababu huduma yake mwenyewe ilikuwa ikidhihirisha hilo Neno. Mnaona? Kwa hiyo hilo lilimfanya nabii.

¹⁶⁴ Kwa hiyo wakati Yesu alipokuja, Yeye alifanya hilo hasa, aliangalia moja kwa moja chini, kasema. Si kwamba tu alimjua, kwa jina, kwamba ni Simoni, Yeye alimjua baba yake, Yona, pia. Naye alijua basi kile baba yake alichomwambia, kwamba huyo Masihi atakuwa ni nabii.

¹⁶⁵ Sasa, haikuwa kwa uponyaji. Walishakuwa na uponyaji, lile birika la Bethesda, na kadhalika. Mungu amefanya njia ya uponyaji kwa ajili ya watu Wake, siku zote. Lakini huyu hapa Masihi aliyetambulishwa. Upesi. Yesu, ama . . . Samahani.

¹⁶⁶ Simoni alitambua jambo hilo. Naye Yesu akamwambia, juu ya maungamo yake, jina lake lingeitwa, mwajua, “Petro.”

¹⁶⁷ Ndipo tunaona kulikuwako na mtu aliyesimama pale, anayeitwa jamaa mwingine mdogo, ambaye alitwa Filipo. Naye alikuwa na rafiki; walikuwa wakiyasoma Maandiko pamoja. Ukiwahi kuwa Palestina, angalia mahali walipokuwa wakihubiria. Basi akazunguka kilima hicho, yapata maili kumi na tano. Ndipo akamkuta Nathanaeli chini ya m—mtini, maana Nathanaeli alikuwa na sha—shamba la mizeituni. Na kwa hiyo, akitoka pale, alimpata chini ya mtini akiomba. Akasema, “Njoo, mwone tuliyempata, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.” Kasema, “Njoo. Njoo, uone. Tulimpata.”

¹⁶⁸ Halafu basi, mwajua, hakika, jamaa huyu, akiwa ni jamaa mzuri kwe—kweli, alisema, “Sasa laweza jambo lolote jema kutoka Nazareti?”

¹⁶⁹ Akampa jibu zuri sana ambalo mtu angeweza kumpa mwingine. “Njoo, uone.” “Usikae nyumbani na kukosoa. Njoo, leta Biblia, na tuichunguze.”

¹⁷⁰ Sasa, hapana shaka, wakakizunguka kilima wakizungumza, kasema, “Sasa, unajua, tunajua Masihi ajapo, Yeye atakuwa ni nabii.”

“Loo, naam, Musa alitwambia hilo. Tunamtazamia nabii.”

¹⁷¹ Na, hakika, watu walidhani kwamba, “Masihi akija, kwamba Mungu angeshusha ushoroba, Naye angekuja moja kwa moja kwenye uwanja wa hekalu, na kusema, ‘Kayafa, nimewasili.’” Lakini Mungu hafanyi mambo namna hiyo.

¹⁷² Yeye hulifanya rahisi sana. Yeye hulipata tu Kanisa Lake. Hilo ndilo analotafuta, Kanisa Lake.

¹⁷³ Kwa hiyo tunaona, ya kwamba yeye alisema, “Unamjua maskini yule mzee mvua samaki uliyemuuzia samaki, ama aliyekuuzia samaki, wakati mmoja, hakuwa na elimu ya kutosha kutia sahihi jina lake kwenye ile risiti?”

“Naam. Simoni.”

¹⁷⁴ “Yeye alimwambia jina lake lilikuwa ni Simoni, na akamwambia kwamba—kwamba baba yake alikuwa ni nani. Vema, haitanishangaza akikwambia wewe ni nani wakati utakapokuja.”

“Vema, tutaenda tukaone.”

¹⁷⁵ Akaja mbele ya Yesu, popote pale, labda kwenye mstari wa maombi, au chochote kile, basi akaja pale. Yesu, akiwaombea wagonjwa. Ndipo akamwangukia. Akasema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli ambaye hamna hila ndani yake.”

¹⁷⁶ Jamani, hilo lilimtoa pumzi. Akasema, “Rabi,” hiyo inamaanisha mwalimu, “uliniona lini? Ulinijua?”

¹⁷⁷ Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.”

¹⁷⁸ Hilo lilitosha. Akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli.” Mnaona? Mtu huyo alikuwa amefunzwa kwelikweli. Alijua ya kwamba Masihi huo ungekuwa ndio u—utambulisho, maana ilibidi awe ni nabii. Mnaona? Maana, ilibidi awe ni Neno. Wala hawakuwa na mmoja kwa muda wa miaka mia nne, kwa hiyo huyu hapa Mtu aliyejitambulisha Mwenyewe, kikamilifu. Huyo alikuwa ni Yesu, jana.

¹⁷⁹ Sasa, tungeweza kuwapitia watu wengi zaidi, bali tuwaruke tu kwa wakati huu.

¹⁸⁰ Kulikuwako na matabaka matatu ya watu duniani, hao ni wana watatu wa Nuhu: Hamu, Shemu, na Yafethi; na hao walikuwa ni Myahudi, Msamaria, na Mmataifa. Sasa, sisi Wamataifa, Anglo-Sakson, hatukumtarajia Masihi yeyote. Tulikuwa na rungu mgongoni mwetu, na tukiziabudu sanamu, Warumi, na kadhalika kama tulivyokuwa. Lakini Wasamaria walikuwa wakimtaazama Masihi.

¹⁸¹ Naye huja tu kwa hao wanaomtarajia. Mungu daima hufanya hivyo. Yeye huja kwa walio Wake. Sasa angalieni.

¹⁸² Yeye alikuwa akishuka kwenda Yeriko, bali alikuwa na sababu iliyombidi kurudi apitie Samaria, Naye akaja kwenye mji jina lake Sikari. Na wakati alipowatuma wanafunzi Wake, kununua chakula, alikuwa ameketi pale. Ndipo mwanamke, labda maskini mtu mrembo ukimwangukia, alikuja kisimani kama saa tano. Maana, asingekuja asubuhi pamoja na wanawali

wengine waliokuja, na kwa hiyo akatokea. Alikuwa—alikuwa na sifa mbaya. Tunajua hiyo ni nini. Na kwa hiyo, yeye, labda nywele zake zikining'inia usoni mwake. Basi akaja, kuweka mtungi wa maji chini. Ulikuwa ni kama mtungi wenye vishikio. Akaweka winchi juu yake, kuushusha.

¹⁸³ Akasikia mtu fulani akisema, “Nipe maji ninywe.” Ndipo akaangalia huko. Akamwona mtu mwenye umri wa makamu amesimama pale, ameketi pale ameegemea ukuta, mandhari fulani yanayofanana na haya hapa. Naye alikuwa ameketi kule akiegemea mizabibu. Kisima hicho cha mji kingali kiko vile vile leo. Basi akasema, “Nipe maji ninywe.”

¹⁸⁴ Naye alikuwa ni Myahudi. Kwa hiyo, walikuwa na ubaguzi kule, pia, kwa hiyo kasema, “Si ninii. . .Hatuwezi. Haina haja. Haikupasi kufanya hivyo. Wewe ni m—wewe ni. . .Wewe ni Myahudi, nami ni mwanamke wa Samaria. Sisi, hatuna uhusiano mmoja kwa mwingine.”

¹⁸⁵ Akasema, “Lakini, kama ulijua ni Nani uliyekuwa ukisema Naye, ungeniomba maji unywe. Ningekupa Maji usije hapa kuyachota.” Mnaona, kile alichokuwa akijaribu kufanya? Kuwasiliana na roho yake, sasa. Mnaona?

¹⁸⁶ Kwa hiyo, akasema, “Mbona, tunaabudu kwenye mlima huu. Nanyi mnasema, ‘katika Yerusalemu.’”

¹⁸⁷ Nao wakaendelea, wakazungumza kidogo. Hatimaye, akapata ilipokuwa shida yake. Alikuwa na waume wengi mno. Akasema, “Nenda kamwite mume wako, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

¹⁸⁸ Akasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, naye yule unayeishi naye siye wako.” Ulisema. . .

Basi angalia tofauti kati yake na hao makuhani.

¹⁸⁹ Wakati hao makuhani walipoona hilo likifanywa, iliwabidi kulijibu kusanyiko lao. Lilikuwa limetendeka. Mnaona? Hao, iliwabidi kusema jambo fulani, kwa hiyo wakasema, “Mtu huyu ni Beelizebuli, mpiga ramli, namna fulani ya ibilisi.” Kasema, “Yeye hufanya hayo kwa nguvu za Beelizebuli.” Hivyo ndivyo makuhani walivyosema.

¹⁹⁰ Maskini mwanamke huyu alisema nini? “Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Tunajua, ajapo Masihi, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake. Hivyo ndivyo atakavyofanya. Yeye atakuwa ni Nabii.”

¹⁹¹ Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.” Loo, jamani! Hilo lilitosha. Mnaona?

¹⁹² Huyu alikuwa ni Yesu Kristo jana. Huyu angekuwa ni Yesu Kristo leo, na awe hata milele. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivyo ndivyo alivyo. Yeye ni Neno

lililodhihirishwa, na Neno la siku hiyo huja na kujitambulisha Lenyewe.

¹⁹³ Na, sasa, Yeye alisema atafanya hivyo tena, kurudi, huyo nabii. Yeye hawezi kuwapita manabii Wake, maana ni Neno. Sasa, Yeye alikufa kwa ajili ya utakaso wetu, akamtuma Roho Mtakatifu kurudi juu yetu, sasa angalieni, kufanya hizo kazi. Sasa, nabii alisema, “Kutakuwako na siku ambayo haitakuwa mchana wala usiku, bali wakati wa jioni itakuwa Nuru.”

¹⁹⁴ Sasa jua huchomoza mashariki na kutua magharibi. Kijeografia, hivyo ndivyo lifanyavyo. Ustaarabu umesafiri pamoja na jua, na Injili vile vile. Kumbukeni, Injili ilianza huko Uropa; ikavuka bahari, ikaingia—ikaingia Ujerumani; kutoka Ujerumani, ikaingia Uingereza; kutoka Uingereza, ikavuka mlangobahari ikaingia Marekani kwenye Pwani ya Mashariki, na tayari imeenda Magharibi. Sasa, kama ikienda mbele zaidi, inarudi Mashariki tena. Tuko mwisho.

¹⁹⁵ Sasa kumekuwako na siku, wakati Mwana huyo alipochochoza huko nyuma hapo mwanzo, M-w-a-n-a wa Mungu akaja duniani. Sasa, Yeye amehidiwa tena katika wakati wa jioni. Sasa, tumekuwa na siku ya utusitusi. Tumekuwa na mikutano mikuu. Tumewaponya wagonjwa. Tumekuwa na nyakati nzuri sana. Nasi tumejiundia madhehebu, na shule, na hospitali, na seminari, ambazo ni sawa, siku tu yenye huzuni. Lakini aliahidi, “Kabla tu usiku haujaingia, itakuwa Nuru.”

¹⁹⁶ Sasa, Yesu alisema, katika Luka Mtakatifu mlango wa 17, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Sasa sikilizeni kwa makini. Ninafunga. “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Sasa, sote tunajua jambo hilo. Sasa, Yeye alisoma Biblia ile ile, katika Mwanzo, tunayosoma.

¹⁹⁷ Basi angalieni yale mandhari huko Sodoma. Sasa, katika Sodoma, kulikuwako na matabaka matatu ya watu. Daima kuna matabaka matatu ya watu: hao ni waaminio, wanaojifanya ni waaminio, na wasioamini.

¹⁹⁸ Sasa, huyu hapa Ibrahimu, jina lake lilikuwa limebadilishwa kutoka Abramam likawa Ibrahimu, ambalo lilimaanisha, “baba wa mataifa.” Naye asingempata mtoto mradi tu jina lake lilikuwa ni Abramam. Ilibidi libadilishwe liwe Ibrahimu, kwa kuwa *ham* kweli linamaanisha “baba wa mataifa,” sasa angalieni, “baba wa mataifa.”

¹⁹⁹ Sasa angalieni, mandhari hiyo haijapata kuwekwa, ulimwenguni kote, kama ilivyo sasa hivi. Sasa tunaona kila kitu kilingana na Sodoma. Kama huliadini, ondoa uvuli kutoka kwenye macho yako, utoke ukatembee mtaani kila siku. Angalia, magazeti, popote utakapo. Ni Sodoma, kabisa. Mnaona?

Na hapo alikuwapo Lutu, huko chini Sodoma.

200 Lakini huyu hapa Ibrahimu, alikuwa ni mteule, yule mwenye ahadi, yeye—yeye hakuwa Sodoma. Hakushuka kwenda kule. Alikuwa ameitwa akatoka.

201 Sasa, kuna makundi matatu ya watu. Kulikuwako na mwaminio halisi; na kulikuwako na mwenye uvuguvugu, ambaye mwalimu yeyote atakwambia kwamba Lutu aliliwakilisha kanisa la kawaida lililokuwa Sodoma; na kulikuwako na Wasodoma basi. Sasa angalieni. Kabla tu ya . . . Walikuwa . . .

202 Ibrahimu na Lutu walikuwa wakimtarajia mwana aliyeahidiwa, wa kimiujiza. Hiyo ni kweli? Je! huyo ndiye kanisa linamtarajia leo hii? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kurudi kwa huyu Mwana, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, tunamtarajia aje.

203 Sasa angalia hali ya mambo. Kila mtu atakubali iko katika hali ya Sodoma. Nilipitia California, hapa hivi majuzi, nikachukua gazeti la juma, ama la kila siku, nikasoma ambapo, “Walawiti walikuwa wameongezeka asilimia sitini, katika mwaka uliopita.” Mnaona? Loo, jamani! Ni huzuni. Mnaona? Ni kwa sababu tu wanawake wamejianika vibaya sana. Hiyo ni kweli. Na wamo tu mtaani, uchi. Na ni—ni fedheha kweli. Lakini Biblia ilisema wangekuwa hivyo. Na hata kwa wanaume, ni kwamba tu wame—wame—wamebadilika. Mnaona? Na itakuwa mbaya zaidi. Katika mingine, mingine, kama ulimwengu ungesimama kwa miaka mingine hamsini, ulimwengu mzima ungeingia wazimu kabisa. Angalia akili timamu kutoka kwenye miaka arobaini, kutoka miaka ishirini iliyopita, hadi wakati huu. Mnaona?

204 Sasa angalia mandhari hii. Huyu hapa Ibrahimu, mteule, aliyeitwa atoke hapa sasa. Halafu kuna Lutu huko chini Sodoma. Ndipo Malaika watatu wakaja. Malaika wawili walishuka wakaenda, kuzungumza na Lutu, nao wakalihubiri Neno, na kujaribu kumwondosha Lutu huko. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Lakini Huyu aliyebacki nyuma na Ibrahimu, hakujaribu kumwondoa Ibrahimu kutoka kwa chochote, maana yeye tayari alikuwa ametoka. Mnaona? Alikuwa ametoka.

205 Lakini angalia alifanya ishara ya namna gani. Sasa angalieni. Alikuwa ameketi ameelekeza mgongo Wake hemani, naye Sara alikuwa hemani, nyuma Yake. Hakuwa amemwona kamwe, bado. Pia kumbukeni, siku moja ama mbili kabla ya hapo, jina lake lilikuwa ni Abramu; na, la mke, yeye alikuwa ni Sarai. Sasa yeye ni Sara, S-a-r-a. Mume ni I-b-r-a-h-i-m-u. Akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” S-a-r-a.

Kasema, “Yuko hemani, nyuma Yako.”

206 Akasema, “Nitakuzuru majira haya mwakani.” Sasa, alikuwa amemtarajia mtoto huyo kwa miaka ishirini na mitano.

Mke yuko karibu miaka mia moja sasa. Mume ana mia moja. Mke ana tisini. Kasema—kasema, “Nitakuzuru majira haya mwakani, nawe utampata huyo mwana.”

²⁰⁷ Ndipo Sara, kwa namna fulani akachekeka, mwajua, kisirisiri. Akasema, “Ati mimi, mwanamke mkongwe?” Mnaona? Kama... Sisi ni hadhara iliyochanganyikana, bali mnajua ninalomaanisha. Kama mume na mke, uhusiano wa kijamii ulikuwa umepita kwa miaka, na miaka, na miaka, mnaona, maana mume alikuwa na mia moja na mke tisini, umri mkubwa mno. Kasema, “Ati mimi nipate raha na bwana wangu, Ibrahimu, naye ni mzee, pia?” Mnaona?

²⁰⁸ Ndipo Mtu huyu, akiwa ameuelekeza mgongo wake kwenye hema, akasema, “Kwa nini Ibrahimu...” Ama, “Kwa nini Sara akachekeka hemani, akisema mambo haya yasingewezekana?”

²⁰⁹ Ibrahimu alimwita, “Elohimu.” Huyu alikuwa ni Mungu. Elohimu ni—ni “Yeye adumuye Peke Yake,” mnaona, anayejitosheleza kwa yote, anayedumu peke yake. “Hapo mwanzo Mungu...” Hebu chukua neno hilo Mungu, liangalie huko nyuma, vile vile, limetafsiriwa vile vile, “Elohimu.” Mwenye... Huyu hapo Elohimu akidhihirishwa katika mwili, aliyekuwa amekula nyama ya ndama, akanywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, na akala mkate. Kisha akaketi, akizungumza na Ibrahimu. Naye Ibrahimu alijua angeweza kutambua yale yaliyokuwa kwenye mawazo ya Sara huko nyuma, na huyo ndiyo sababu yeye alijua ya kwamba huyo alikuwa ni Elohimu.

²¹⁰ Yesu alisema, angalieni, “Katika siku atakapofunuliwa Mwana wa Adamu, akifunuliwa katika siku za mwisho, itakuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Mungu akidhihirishwa katika Kanisa Lake, wanadamu, akijifunua Mwenyewe, mnaona, katika mwili wa kibinadamu, kama alivyokuwa wakati huo. Sasa angalieni.

²¹¹ Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Katika nyakati zote, tangu kanisa lilipoanza kwa mara ya kwanza, hawajapata kuwa na mjumbe kwao ambaye jina lake liliishia kwa h-a-m, mpaka sasa, G-r-a-h-a-m. Kweli. Huko chini, akiwaita watoke, Oral Roberts, na Billy Graham, mnaona, h-a-m. Kumekuwako na Moody, Sankey, Finney, Wesley, Billy Sunday, wote hao, mnaona, kanisa la kimataifa namna hiyo, kanisa la ulimwengu!...?... Hakujapata kuwapo na moja lililoishia kwa h-a-m mpaka hivi sasa, na huyo ni Billy Graham. Mnaona? Na hizo ni herufi sita, G-r-a-h-a-m, sita, zikimaanisha... Mwanadamu alizaliwa, aliumbwa kwenye siku ya sita. Sita ni nambari ya mwanadamu. Huyu hapo, kwa kanisa la kawaida.

²¹² Ibrahimu alikuwa ni A-b-r-a-h-a-m, herufi saba. Mnaona? Angalieni mandhari hiyo leo hii, na mwangalie yanayotukia. Ibrahimu alikuwa ameona ishara nyingi na maajabu, na kila kitu ambacho Mungu alikuwa amefanya. Vivyo hivyo na Kanisa.

Mmempokea Roho Mtakatifu, mkanena kwa lugha, mkafanya ishara hizi zote na maajabu. Lakini mmeahidiwa, “Kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo itakavyokuwa tena.” “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Yesu Kristo, yeye yule; Mwana yule yule atajitokeza tena jukwaani, katika Kanisa Lake, na atafanya jambo lile lile alilofanya wakati huo, akionyesha ya kwamba Yeye ni Neno lililodhihirishwa. Mnaona? Akiua siri iliyoko moyoni, akifunua na kufanya mambo anayopaswa kufanya. Hilo ni Neno la Mungu hasa.

²¹³ Tunachelewa. Kwa hiyo na tuviinamishe vichwa vyetu, kwa muda mfupi tu, tunapomwangua Yeye na kumwomba alithibitishe Neno Lake.

²¹⁴ Baba wa Mbinguni, wakati usingeruhusu; saa baada ya saa, tungeketi, tukisema, kutoka tu Mwanzo hadi Ufunuo, huu ndio wakati. Ee Bwana, ziara yetu ya kwanza hapa pamoja na kundi hili la watu hapa pwani, ambayo, tunajua ya kwamba siku moja itazama chini ya bahari, wala hapatakuwa na jiwe litakalosalia juu ya lingine. Kutakuwako... Loo, ni wakati wa jinsi gani ulio mbele!

²¹⁵ Jalia, Bwana, katika saa hii ambapo tunatoa ushahidi, jalia Roho Mtakatifu mkuu aje sasa. Nayo maneno haya ambayo nimesema, jalia ayaunge mkono, kwa kuyathibitisha. Yeye anaithibitisha hadhara hii ya kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninii... Na kulitimiza Andiko hilo. Tunajua huninii... Haikubidi kufanya hivyo, Bwana, kuthibitisha ya kwamba ulikuwa ni Mungu. Lakini kama tulivyosoma katika Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, yapata mlango wa 12, haikumbidi kuponya, kuonyesha alikuwa ni Mungu. Lakini aliponya, ipate kutimizwa. Hana budi kulitimiza Neno Lake, Naye anapenda kufanya hivyo. Naye atafanya hivyo, kwa kuwa Yeye ni Mungu. Nami ninaomba, usiku wa leo, sasa, kwamba atalitimiza Neno hili pia, lililoahidiwa kwa ajili ya saa hii. Jalia ndugu zangu wote, na mimi wote, na watu wote walio hapa, na dada zetu, kundi hili la watu wa kupendeza, wauone Uwepo Wako miongoni mwetu sasa. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

²¹⁶ Sasa, kidogo tunachelewa, kwa hiyo tutaita tu ninii... Naam, tumechelewa kweli. Tutatumia dakika zingine kama kumi, ama kumi na tano. Hebu tuwaite tu wachache kwenye mstari wa maombi.

²¹⁷ Kadi za maombi, uliwapa A? Naam, A. A, namba moja, hebu tupate mmoja kuninii... Ni nani aliye na kadi ya maombi A, namba moja? Inua mkono wako. Kama unaweza kutembea... Ni kadi ndogo, iliyo na namba juu yake. A, namba moja, inua mkono wako. Mnataka kusema haimo kwenye wasikilizaji?

218 Vema, hapana shaka ulikosea. Kadi ya maombi A, moja? [Mtu fulani anasema, “Papa hapa, Ndugu Branham.”—Mh.] Vema, loo, ndiyo? Vema. A, mbili?

219 Njoo papa hapa, ukitaka, mama. Kuja papa hapa. Vema, hebu tuone, anaweza kupitia hapo? Nina shaka. Loo, naam, yote ni kupitia hapo shimoni. Vema.

220 A, namba mbili, ni nani aliye na hiyo? Tatu? Inua mkono wako. Kama huwezi kuja sasa . . . Hiyo ndiyo sababu tunawaita, mmoja mmoja, huenda ikatubidi kuwabeba kuwaleta humu ndani. Tatu? Nne, ni nani aliye na nne? Tano? Hapa chini, mama. Njoo huku.

221 Sita, kadi ya maombi namba sita. Huyu ndiye huyo mama anayesimama hapa juu, amevaa maskini jaketi nyeupe? Una sita? Saba? Wakati mwingine wao ni viziwi, hawawezi kusikia. Wakati mwingine hawawezi kutembea. Saba. Nane. Sikuona nane akisimama. Waweza kuinua mkono wako? Vema. Tisa. Kumi. Vema.

222 Hebu tungojee tu hapo kwa dakika moja, maana tunachelewa sasa. Hebu tuwaone hawa kwa dakika moja. Shikeni tu kadi zenu. Tutawaita, mmoja mmoja, mnaona, lakini kaeni tu mstarini.

223 Sasa, ni wangapi humu ndani wasio na kadi ya maombi? Inua mkono wako, useme, “Mimi ni mgonjwa. Sina kadi ya maombi.” Inua mkono wako, juu tu sana nipate kuuona. Nadhani ni kila mahali. Sasa, angalieni. Ninataka kuzungumza nanyi kwa dakika moja tu wakati wakijipanga mstarini.

224 Kulikuwako na mwanamke, tunasema, katika Biblia, pia, hakuwa na kadi ya maombi. Na, bali alikuwa na imani. Na kwa hiyo a—akasema, “Kama ninaweza kugusa vazi Lake, nitaponywa.” Ni wangapi wanaojua hadithi hiyo? Hakika. Basi wakati alipoligusa vazi Lake, Yeye aligeuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

225 Vema, Petro aliwazia hilo lilisikika kana kwamba ni kuchanganyikiwa. Akasema, “Mbona, kila mtu anakugusa. Ati unasema ni nani ‘aliyekugusa’? Mbona, hawatakuwazia mema sana, kama ukininii . . .”

226 Akasema, “Lakini naona nimekuwa mnyonge.” Nguvu zilimtoka. Ndipo akageuka na kuiangalia hadhira Yake mpaka akampata mwanamke huyo. Basi akamwambia, kwamba, kutokwa kwake na damu, imani yake ilikuwa imemponya. Ni wangapi wanaojua hiyo kuwa ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

227 Sasa, hivi ndio kwanza nimalize kusema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele”? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivi Biblia inasema, kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu”? [“Amina.”]

Hiyo ni kweli? [“Amina.”] Basi Yeye angetendaje leo? Angetenda jinsi alivyotenda jana. Hiyo ni kweli? Sasa, kumbukeni, ungali unaweza kumgusa. Unaona? Maandiko hayawezi kusema uongo. Mnaona?

228 Sasa, kitu pekee kisicho hapa ni mwili Wake unaonekana. Lakini wewe. . . Yeye Ndiye Mzabibu, nawe ni tawi. Unaona? Hiyo. . . Wewe ni tawi. Wewe ndiwe unayetenda kazi.

229 Mimi na wewe tunatenda kazi pamoja. Sasa, haidhuru angenipaka mafuta jinsi gani, hana budi kukupaka mafuta, pia. Unaona? Maana, haina budi kuwa—haina budi kuwa ni kivuli na halisi pia, kuiwasha taa. Kwa hiyo, sasa, hu—huna budi kuamini, pia.

230 Sasa, wewe usiye na kadi ya maombi, angalia tu huku na kusema, “Bwana Yesu, mtu yule hanijui. Kuna jambo moja la hakika, yeye hanijui. Lakini ninaugua kitu fulani, na—na jalia ageuke na kuniambia habari zake, kama Yesu alivyofanya kule. Nami ninajua yeye hanijui, kwa hiyo haina budi kuwa ni Wewe, kwa hiyo basi ni—ni—nitaliamini.” Mnaweza kufanya hivyo? Mtaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Vema. Ombeni tu sasa.

231 Nitaichukua hii. Inaonekana kana kwamba simu hii ni ninii zaidi. . . Ni sawa. Kwa namna fulani ilikuwa kidogo ni hai kuliko awali.

232 Sasa, ndugu, hii ndiyo Injili mnayohubiri. Mnaona? Nanyi niombeeni.

233 Sasa, sasa kila mtu awe na kicho tu mwezavyo, kisha mwangalie huku. Pia uamini kwa moyo wako wote. Amini tu, kila. . . ki—kila kitu tu kilicho ndani yako. Amini. Wala usitie shaka. Usitie shaka, hata kidogo.

234 Sasa, sasa huyu hapa mama amesimama hapa. Nadhani sisi ni ninii. . . Mimi na yeye hatufahamiani. Simjui. Na. . . [Dada huyo anasema, “Mara moja kabla ya hapo.”—Mh.] Uliniona mara moja? [“Mara moja hapo mbeleni, huko Clearwater.”] Ati wapi? [“Clearwater, naamini ndiko.”] Clearwater? Ni muda gani huo? [“Ama, St. Petersburg, moja.”] Naam. St. Petersburg. Naam. Nimekuwa huko—huko St. Petersburg. [“Naam.”] Imekuwa ni miaka kadhaa iliyopita. [“Ndiyo.”] Vema, sasa, labda ukiketi kwenye wasikilizaji, ama kitu kama hicho. [“Ndiyo.”] Hiyo ni. . . Nisingekujua, wajua, wala kujua lolote kukuhusu.

235 Kwa hiyo sasa, hapa nikizungumza nawe, ingekuwa tu ni kama Bwana wetu, na yule mwanamke walivyokutana, kisimani, wakati ule, unaona. Na—Naye akazungumza naye kwa dakika moja, apate kujua shida yake ilikuwa wapi. Naye akaipata, kwa sababu, unaona, a—alikuwa ni mwanadamu naye alikuwa na uhai, roho. Naye alikuwa ni Mungu, na alikuwa na Roho wa Mungu, alikuwa ndani Yake. Na kulikuwa na shida fulani na

mwanamke huyo, ndipo Baba akamwonyesha kwamba ilikuwa ni nini.

²³⁶ Mwajua, Yeye alisema, hakufanya neno mpaka Baba amwonyeshe, kwanza. Mwajua, hiyo ni Yohana Mtakatifu 5:19. Hiyo ni kweli, ndugu? [Kina ndugu wanasema, “Amina.”—Mh.] Akasema, “Mimi...” Si—si kile alichooona... Ilimbidi kukiona, kwanza. Yesu kamwe hakutenda neno moja mpaka alipoona ono kwanza. Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Yohana Mtakatifu 5:19. “Sitendi neno mpaka Baba... Nimwone Baba akilitenda kwanza.” Mnaona? Sasa, kama Yeye...

²³⁷ Sasa, hakika, mimi si Yeye, nawe siye yule mwanamke. Bali angali ni Mungu yeye yule. Mnaona? Nasi tupo hapa, tukikutanika kwa kusudi fulani.

²³⁸ Sasa, mwanamke huyu hapa, kama mnavyoweza kufahamu, hatufahamiani. Miaka kadhaa iliyopita, alikuwa ameketi kwenye wasikilizaji, kama vile mlivyo usiku wa leo, nilipokuwa St. Petersburg, alisema, mkutanoni. Sina njia... Simfahamu kabisa, sijui lolote kumhusu, Naye Baba wa Mbinguni anajua hilo. Lakini sasa yupo hapa kwa kusudi fulani. Huenda akawa hapa kwa ajili ya mtu mwingine, shida ya kifedha, shida ya nyumbani. Huenda akawa ni mgonjwa, yeye mwenyewe. Mimi—mimi... Huenda amesimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Sijui ni nini kilichomleta hapa. Mnaona? Yeye ni mwanamke tu.

²³⁹ Sasa vipi kama alikuwa ni mgonjwa, nami ningekuwa kama ndugu yetu muungwana, Ndugu Oral Roberts, na niweke mikono juu yake, niseme, “Bwana akuponye na akupe afya,” nawe uondoke ukiamini hilo. Hilo ni sawa. Hilo ni ninii tu... Hilo ni Maandiko. Na kama ukiliamini, utapona. Unaona? Lakini, unaona, hiyo ni huduma ya Ndugu Roberts; hiyo siyo yangu. Mnaona?

Sasa huu ni mtazamo mwingine, mmoja hapa juu kwenye wakati wa mwisho.

²⁴⁰ Sasa Yesu alikuwa ni nani? Yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa kama Yeye alisimama hapa amevaa suti hii niliyovaa, ambayo alinipa, sasa, kama mwanamke huyu ni mgonjwa, je! angeweza kumponya? Iweni waangalifu sasa. Iweni waangalifu. La. Asingeweza kufanya hivyo. Amemponya tayari. Unaona? Unaona? “Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Tayari amemponya. Jambo pekee angaliweza kufanya ni kujitambulisha Mwenyewe kwake, hiyo ni kweli, na kuwajulisha kwamba amefufuka katika wafu, na yu hai. Na sasa, kwamba, Yeye angejitambulisha Mwenyewe. Na jinsi tu angaliweza kufanya hivyo, ingekuwa kama alivyokuwa wakati huo. Angekuwa ni Nabii. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁴¹ Sasa, mimi, isingekuwa ni mimi, maana si—sijui lolote kulihusu, kwa hiyo hilo linanitoa mimi. Lakini itabidi iwe ni Yeye. Kwa hiyo kama sisi ni tawi Naye ni Mzabibu, Yeye anamtuma Roho Wake ndani yangu, kunifanya nijue jambo fulani lako, ama kitu fulani unachotaka, kile umekuwa, kile ulicho, ama kile utakachokuwa, ama kitu kingine. Utajua kama ni Kweli ama sivyo, kama imetendeka tayari. [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Kwa hiyo hilo linapaswa kukufanya uone kweli kwamba Yeye yu hai na yuko pamoja na sisi leo hii. [“Ndiyo.”] Unaona?

²⁴² Hilo lingewafanya muamini, kama angelifanya? Sasa inueni mikono yenu, ninataka kujua, kwa hiyo wewe umwahidi Mungu, “Litanifanya niamini.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Kuwa Yeye ni, Yeye . . . Mnaona?

²⁴³ Sasa, nimekuwa nikizungumza juu Yake kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, je! Yeye, Yeye yu hai? Jambo ndilo hilo. Je! Yupo hapa? Tumepaza sauti, na kuhisi kitu Fulani.

²⁴⁴ Ni kama tu ikiwa mtu hajawahi kuwa na macho, naye akatoka nje na kulihisi jua, asingejua lilikuwa ni kitu gani. Kilikuwa ni kitu chenye joto. Lakini kama angeweza kuona, angeona kilikuwa ni kitu gani, angesema hilo ni jua. “Jua ni nini?” Kwa mtu mwingine, kamwe hajaona, labda, hili, hakuna mtu aliyewahi kuwa na hisi ya kuona hapa awali.

²⁴⁵ Sasa, huu ni utambuzi. Na kitu ambacho mmekuwa mkikisifu na kukifurahia, Hiki hapa kinajidhihirisha Chenyewe nanyi mnaona kwamba ni Kitu gani. Mnaona? Sasa Huyu hapa, huku Biblia hii ikiwa imewekwa hapa, na kundi hili zuri la ndugu hapa na kila mahali.

²⁴⁶ Sote wawili hatufahamiani. Sasa Bwana Yesu na afunue. Sasa, kuponya, ama kumpa anachotaka . . . Kama ilikuwa ni pesa, itabidi iwe ni chache sana, maana sina nyingi sana; bali ningekupa; ningefanya vizuri niwezavyo. Lakini—lakini, sasa, kuponya, nisingefanya hivyo. Mnaona? Kungepaswa kutoke Kwake. Lakini, sasa, kama Yeye ataniambia jambo fulani kukuhusu; nawe unajua sijui kitu. Na kama angeniambia kitu fulani kukuhusu, ingeongezea imani yako, sivyo, kukufanya uamini ya kwamba Yeye yupo hapa? [Huyo dada anasema, “Ndiyo. Ndiyo.”—Mh.] Sasa, na afanye hivyo.

²⁴⁷ Katika Jina la Yesu Kristo, nachukua kila roho humu ndani, chini ya mamlaka yangu sasa, kutoa ushahidi kwa Neno hili la Mungu. Ninaninii tu . . .

²⁴⁸ Iweni mkiomba sasa. Mnaona? Mnasema, “Kwani ulikuwa ukingojea nini, Ndugu Branham?” Ni wangapi wamepata kuona picha ya ile Nuru? Hiyo ndiyo Yeye . . . Hii hapa, papa hapa sasa. Ipo papa hapa sasa. Sasa asingeweza kujificha, kama angejaribu. Asingeweza sasa. Yeye ni mtu mzuri. Hana kitu cha kuhofia. Anajua jambo fulani linaendelea, pia.

249 Lakini, kile mwanamke huyu anachotaka, yeye ana hali ya kudhoofisha inayomjia, yabisi kavu inayomjia mwanamke huyu. Hiyo ni kweli. Ndiyo hiyo. Mnaona? [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Naam. Inua mkono wako kama hiyo ni kweli, kama ni yabisi kavu. Sasa je! uniamini, naweza kukwambia mahali yabisi kavu inapokuuma sana? [“Ndiyo.”] Ni katika mifupa yako. Hiyo ni kweli. Na una tatizo lingine. Unaamini Mungu anaweza kusema ni nini? Una kivimbe. [“Ndiyo.”] Naam, bwana. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. Unaamini Mungu anaweza kuniambia hicho kiko wapi? [“Ndiyo.”] Kiko kwenye titi lako. [“Naam.”] Hiyo ni kweli. Punga mkono wako namna *hii*. Sasa, unaona, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa unaamini kwa moyo wako wote? [“Naam.”] Endelea, wala hakitakusumbua tena, basi. Nenda tu, amini kwa moyo wako wote. Hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya. Unaona? Nenda zako na uamini. Unaona?

250 Sasa, hilo, mnaona, simjui mwanamke huyu. Sasa, mnajua ni muda gani niliozungumza nanyi, zaidi ya dakika arobaini na tano. Nimedhoofika zaidi sasa, kutokana na hilo, kuliko nilivyokuwa kwenye mazungumzo hayo yote. Mnaona?

251 Sasa huyu hapa mama. Hatufahamiani, nadhani. Hatujuani, bali Mungu anatumia sote wawili. Sasa, kama Yesu ataniambia jambo fulani kukuhusu, ambalo unajua silijui, hilo lingekusaidia kuwa na imani katika yale utakayoomba? [Dada anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Lingewasaidia wasikilizaji sasa? Mnaona?

252 Sasa, kumbukeni, Yeye anaahidi yale mandhari kama Sodoma hasa. Mnauona Sodoma; mnamwona Billy Graham, kila kitu, vile vile hasa. Sasa liangalieni kundi la Ibrahimu hapa juu, mnaona, U—Uzao wa kifalme wa Ibrahimu. “Tukiwa wafu katika Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu.” Hiyo ni kweli, ndugu. Sisi sote ni . . .

253 Ni kivimbe. [Huyo dada anasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Upasuaji hausaidii kitu. Nawe unahitaji ninii . . . Una matatizo nao, wakati wote. Unaamini kitakuacha sasa? [“Amina.”] Vema. Mungu akubariki. Kama ulivyoamini, ndivyo itakavyokuwa kwako. Vema. Kuwa tu na imani sasa. Usitilie shaka, unaona. Kuwa na imani, mama. Vema. Mwingine . . . Hicho kinaondoka. Unaona?

254 Sasa wewe njoo. Wewe ndiwe mgonjwa anayefuata. Sasa, hatufahamiani, mmoja kwa mwingine. [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Hatufahamiani . . . Sijapata kukuona hapo awali. Wewe ni ninii tu . . . [“Sijapata kukuona maishani mwangu.”] Kamwe hujapata kuniona maishani mwako, wala mimi sijapata kukuona maishani mwangu. Sisi ni watu wawili tu waliokutana.

255 Sasa ni kitu gani hiki? Ni karama. Mnaona? Karama si kitu kama kijiti ama upanga, unaokata nao na kadhalika. Karama ni—ni njia ya kujiondoa njiani. Mnaona? Unaninii tu... Sina budi kujiondoa njiani, ndipo Roho Mtakatifu anachukua mamlaka. Mnaona? Si kile unachochukua na kufanya jambo fulani nacho. Ni karama ya kujiondoa njiani, ndipo Mungu anakutumia. Mnaona? Ukiisha kujiondoa...Kama tu ninii kidogo...

256 Huwezi kulielezea, maana usingeweza kumwelezea Mungu. Tunamwamini Mungu. Hatumwelezei; hatuwezi. Unamjua Mungu kwa imani, wala sio kwa sayansi, ama njia nyingine yoyote. Humthibitishi kisayansi. Unamwamini tu. Usingeweza kuthibitisha kwamba upendo ni kitu gani. Usingeweza kuthibitisha furaha ni nini. Silaha zote za Mungu, upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, unyenyekevu, subira, hizo zote ni za kimbinguni. Mnaona? Huwezi kuzithibitisha, bali unajua unazo. Mnaona? Jambo ndilo hilo, kwa hiyo unajua hilo mwenyewe.

257 Mama huyu ni mchovu sana. A—ana tatizo fulani kinywani mwake, ndani ya kinywa chake. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Na umeshikwa na kansa, unahofia ni hivyo. Hiyo ni kweli.

Sasa mnasema, “Ulibahatisha hilo.”

258 Sikubahatisha, hata. [Dada huyo anasema, “La.”—Mh.] Hubahatishi mambo hayo. Angalia, angalia hapa tena. Wewe ni mtu mzuri sana. Jambo fulani lilikupata wakati huo. Lakini ninaninii tu...Hapa, umekuwa na ajali ya motokaa, pia. Sivyo? [“Hiyo ni kweli.”] Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. [“Amina.”] Hilo, unaona sasa, ni—nisingejua hilo. [“La.”] Vema, basi, nenda zako, ukishangilia. Mwamini tu Mungu. Amina. Liamini.

Njoo sasa. Unaamini.

259 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, ninyi mlilo huko nje, anzeni tu kuamini kwa moyo wenu wote. Msitilie shaka, bali aminini kila neno kwamba ni kweli. Mnaona, huyo ni Yeye. Huyu ni Bwana wenu. Yuko moja kwa moja miongoni mwenu. Mnaamini hilo, huko nje? [“Amina.”]

260 Sasa, hatufahamiani, mmoja kwa mwingine, nadhani. Sikujui, wala hunijui. Vema, hilo ni zuri. Sasa hilo linalifanya kusudi...Kamwe sijapata kuwa hapa awali, wajua. Tuko tu hapa mjini. Na—nawe ni mhitaji, ama chochote kile. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia haja ya—yako, ama chochote kile? Utaniamini. Si kwa ajili yako. Ni kwa ajili ya mtu mwingine. [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Huyu ni mjukuu. [“Ndiyo.”] Na huyo mjukuu kwa namna fulani amedumaa. [“Ndiyo.”] Hiyo ni kweli kabisa. Yuko mahali

pengine. Hayuko hapa. Kitu kama New Meksiko. [“Naam.”] Ama nini. . . Ni huko New Meksiko. Huko ndiko aliko. Nenda, amini sasa, kwa moyo wako wote.

²⁶¹ Hatufahamiani, mmoja kwa mwingine. Sisi, mara yetu ya kwanza kukutana. Lakini. . . Vema.

²⁶² Mtu anayeketi pale pale, kitu hiki, kinaenda namna *hii*, nakiangalia, unaugua ugonjwa wa tumbo, bwana. Hiyo ni kweli. Uliketi hapo ukishangaa jinsi hilo lilivyopata kufanywa. Hiyo si ni kweli? Na kuwazia juu ya tumbo lako mwenyewe. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Simjui mtu huyu, sijapata kumwona maishani mwangu. Vema. Una tabia unayotaka kuacha, kuvuta sigara. Unataka kuacha huko kuvuta sigara? Huko ndiko kunakoathiri tumbo lako, unapovuta sigara; nikotini inashuka chini, inalitupilia tumbo lako kwenye mshtuko wa ghafla. Sijapata kumwona mtu huyu maishani mwangu, naye huyo hapo. Sasa simama, kama hiyo ni kweli, bwana. Nakanusha sigara kutoka kwako. Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukapate afya. Sasa, sijapata kumwona maishani mwangu. Yeye aligusa nini? Alimgusa Bwana.

²⁶³ Jambo lingine, mama anayeketi karibu nawe hapo, mpendwa, ana matatizo ya tumbo, pia. [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Hiyo ni kweli. Unataka kuachana na matatizo yako ya tumbo, mama? Mnaona, Roho, ni siku ya mwisho. Hivi hamwioni ile Nuru ikining’inia pale pale kuwazunguka, karibu nao? Hiyo ni kweli. Vema. Hiyo ni kweli. Sasa wewe nenda, amini, wasiwasi wako utakuacha. Na huo ndio uliosababisha tatizo lako la tumbo. Hiyo ni kweli. Amini kwa moyo wako wote sasa. Vema.

²⁶⁴ Jambo lingine, yupo mama mwingine anayeketi hapo, karibu nawe, ana mzio. Kama hiyo ni kweli, simama, mama. Hiyo ni kweli. Simama kwa miguu yako na ulikubali. Na, vema, unaamini ya kwamba Mungu atakuondolea? Basi unaweza kupata ulichoomba.

²⁶⁵ Sasa, sijapata kuwaona maishani mwangu. Na hivyo ndivyo ilivyo hasa. Waligusa nini? Walimgusa Ku—Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wao. Yeyote wenu huko, aminini jambo lile lile. Aminini tu.

²⁶⁶ Akiketi pale, mtu anataka ubatizo wa Roho Mtakatifu. Anatafuta kazi, pia. Je! unaamini kwamba Mungu atakupata Roho Mtakatifu, na kukupa kazi? Sasa inua mkono wako; papa hapa, unayeketi pale umevaa shati jeupe. Vema. Sijawahi kumwona maishani mwangu, bali ndivyo hasa alivyokuwa akiwazia. Kama hiyo ni kweli, pungua mkono wako *hivi*.

²⁶⁷ Sasa hivi hamwoni? Neno la Mungu huyatambua mawazo na makusudi ya moyo. “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Huyo ni Yeye huko nje. Mnajua isingekuwa ni mimi. Siko huko. Niko yadi ishirini kutoka kwake. Bali alimgusa Kuhani

Mkuu. Loo, wazo la Kristo kuwapo, ewe rafiki, je! waweza kulifahamu?

²⁶⁸ Samahani, mama. Sina budi kufuatilia tu, wajua, mvuto kama huu wa imani. Ulianza huko nje, sasa ni vigumu kuuachilia, unaona. [Dada huyo anasema, “Hiyo ni sawa.”—Mh.] Vema. Wewe ni mwaminio. [“Naam, bwana.”] Nawe unaamini ya kwamba upasuaji huo ambao uko karibu kufanyiwa, je! unaamini kwamba Mungu anaweza kukuondolea huo kabla ya kufanyiwa upasuaji? Unaamini, pia? [“Nilikuwa nifanyiwe.”] Basi unaamini sasa kwamba . . . Wana huyo binti aliye na namna fulani ya mafua yaletwayo na vumbi, ama kitu kama hicho. Unaamini kwamba Mungu atamponya hayo mafua yaletwayo na vumbi? Unaamini hivyo? Vema. Sasa nenda ukamwekee mikono yako, na uamini kwa moyo wako wote, na Mungu atamponya. Kuwa na imani.

²⁶⁹ Unataka kula chakula chako cha jioni? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Unaamini tumbo lako litakuwa sawa? [“Ndiyo.”] Vema, basi nenda ukale. Bwana Yesu yupo hapa. Vema.

²⁷⁰ Njoo, mlete mama huyo. Kuwa na imani. Usitilie shaka. Njoo, mama. Unaamini Mungu anaweza kuponya kisukari hicho, akupe afya? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, ndugu.”—Mh.] Kwa moyo wako wote, unaamini? [“Amina.”] Vema, basi nenda zako, shangilia na kusema, “Asante, Bwana Yesu,” kwa moyo wako wote.

²⁷¹ Mungu anaweza kuuponya ugonjwa wako wa mgongo, akupe afya. Unaamini hilo? [Dada huyo anasema, “Hakika naamini.”—Mh.] Vema, nenda zako tu, useme, “Asante, Bwana Yesu, kwa moyo wote.” Huna budi kuamini.

²⁷² Njoo, mama. Wewe ni kijana. Lakini, unakufa kwa urahisi, kwa matatizo ya moyo. Lakini unaamini Mungu anaweza kuuponya moyo wako? Basi nenda zako, ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana Yesu.” Na uamini kwa moyo wako wote. Vema.

²⁷³ Njoo, bwana. Umekuwa na wasiwasi, unakupa donda la mmeng’enyoy tumboni mwako. Nenda, ukale chakula chako cha jioni. Yesu Kristo anakuponya. Amini kwa moyo wako wote. Unaamini?

²⁷⁴ Unaamini Mungu anaweza kuponya pumu hiyo? Unayeketi hapo nje, ukiniangalia, umevaa miwani; maskini gauni lenye milia. Mama huyo, unaamini, unayeketi hapo mwishoni? Unaamini Mungu atashughulikia pumu hiyo? Inua mkono wako kama unaamini. Vema. Yeye atakuponya.

²⁷⁵ Unawazia nini juu ya jambo hilo, unayeketi moja kwa moja nyuma yake, bwana? Unaamini unaweza kuuepa upasuaji huo wa kivimbe? Unaamini Mungu anaweza kukiondoa hicho kivimbe na kukuponya, akuponye hicho kivimbe? Unaamini hivyo? Vema, bwana, unaweza kupata wako, pia. Unaona? Vema.

Laiti ungalikuwa tu na imani, wala usitilie shaka, Mungu hakika atakuponya. Amina.

²⁷⁶ Ni wangapi wanaoamini huko nje, kwa moyo wenu wote sasa, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaamini ya kwamba huyo ni Yesu aliyefufuka? [“Amina.”] Sasa, yeyote wenu anajua kwamba nisingefanya hilo. Sijui lolote kuwahusu ninyi nyote, bali Yeye anajua.

²⁷⁷ Sasa Biblia pia inasema hivi. Ni wangapi wenu walio waaminio? Inua mkono wako. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa, Yesu alisema, Maneno Yake ya mwisho kwa Kanisa, wakati akiondoka, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Unaamini hilo? [“Amina.”]

²⁷⁸ Sasa je! mtanifanyia jambo fulani basi? Sasa wekeaneni mikono. Usifanye kitu kamwe ila kuweka mkono wako juu ya mtu anayeketi karibu nawe, huku tu namna hiyo. Basi. Gusaneni tu mkono. Vema.

²⁷⁹ Nataka kuwaulizeni swali. Ninawatakeni mniangalie. Kumbukeni, hakika kama vile Maandiko yanavyosema hili, Ibrahimu hakuona ishara moja zaidi mpaka yule mwana alipotokea. Hiyo ndiyo ishara ya mwisho aliyoona Ibrahimu. Daima kuna ishara. Hebu niwaambie, Kanisa, hii hapa ishara yenu ya mwisho. Kuonekana kwa Mwana kutakuwa ni hivi karibuni sana. “Kwenye saa msiyowazia, watanyakuliwa.” Watu wataendelea moja kwa moja wakihubiri, wakidhani wanaokoka, na kila kitu. Yeye ataninii. . . Kama tu ilivyokuwa katika kuja kwa Yohana, wote, waliendelea tu mbele, wakati ukaisha. Kumechelewa kuliko tunavyodhania.

Sasa mmewekeana mikono mmoja kwa mwingine.

²⁸⁰ Nanyi mmeona kitu ambacho Yesu aliahidi katika siku hizi za mwisho, angekifanya, na hapa amegeuka moja kwa moja na kufanya yale hasa aliyosema.

²⁸¹ Sasa, unasema wewe ni mwaminio. Ninaamini hilo. Sasa, umeweka mkono wako juu ya mtu fulani.

²⁸² Nao uwepo Wake uko hapa sasa. Sasa, huyo ni Yeye. Nimeona mtu akiponywa tu basi, wakati uo huo, huku mkono wake umewekwa juu ya mtu mwingine. Mnaona? Ni—ni vile tu—vile inavyopaswa kufanya.

²⁸³ Lakini, mnaona, inakuja kwenye wakati ambapo kanisa la Laodikia linaendelea. Kama ilikuwa ni katika wakati wa uamsho, inamulika tu na kwenda namna *hiyo*. [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja—Mh.] Lakini, mnaona, ilifikia wakati alipofukuzwa kanisani. Mnakumbuka, hivi majuzi,

wakati lile tetemeko la ardhi? Mnaukumbuka wakati wa kanisa la Laodikia? Yeye yuko nje ya kanisa, akibisha, akijaribu kurudi ndani. Mnaona? Hapo ndipo imefikia, mnaona. Yeye anajaribu kurudi. Anataka kujitambulisha nanyi, kwa ajili ya ma—maombi yenu.

²⁸⁴ Sasa, usijiombee. Mwombee yule uliyemwekea mkono wako, maana wanakuombea. Unaona? Na, basi, amini kwa moyo wako wote. Omba tu jinsi unavyoomba kanisani mwako. Kama unaomba kwa sauti kubwa, omba kwa sauti kubwa; unaomba kimoyo-moyo, omba kimoyo-moyo. Vyovyote mfanyavyo kanisani mwenu, wewe omba.

²⁸⁵ Na useme, “Bwana Yesu, nina hakika ya kwamba niko katika Uwepo Wako sasa. Yule Bwana Yesu mkuu aliyefufuka katika wafu na amejitambulisha Mwenyewe papa hapa kwenye jumba hili la mikutano huku chini kabisa, na, jamani, karibu, ama Tampa, Florida. Niko huku chini kabisa, Nawe huyu hapa kwenye jumba hili la mikutano, usiku wa leo. Pamoja na Roho uliyokuwa nayo ulipokuwa hapa, ukamtuma miongoni mwetu. Nasi tumeona imani yetu wenyewe, ama Ndugu Branham na imani, kupitia kwenye karama aliyopewa, aliyozaliwa nayo. Naye hapa alikuwa na imani, kusimama pale na kujitupilia mbali na kila kitu, pasipo kumjua yeyote wetu. Nawe ukaingia na kuitumia karama hiyo, kwa kuwa alijiachilia tu. Nawe, yeye. . . Ukaitumia. Hapa kulikuwako na watu hapa jukwaani, huku kwenye wasikilizaji, wageni kabisa, Nayo ikalidhihirisha Neno. Neno la Mungu limedhihirishwa, kujua kwamba Yeye ni Neno, yeye yule jana, leo, na hata milele. Wewe huyu hapa! Nami ninakuamini. Nami nimeweka mikono yangu juu ya mtu fulani, nao wameweka mikono yao juu yangu. Sasa, Uwepo mkuu wa Kristo, mponye mtu huyu.”

²⁸⁶ Nami nitawaombea ninyi nyote. Sasa ninyi ombeaneni, huku nikiwaombea ninyi nyote. Nanyi mtaponywa, kila mmoja wenu, sasa hivi, kila mmoja atakayeamini.

²⁸⁷ Baba wa Mbinguni, wakati kundi hili la watu hapa, usiku wa leo. Nasi tu—tunakushukuru kwa ajili ya Uwepo Wako, Bwana. Huo unatuhibitishia ya kwamba dini yetu ya Kikristo ni sahihi. Dini ya Kiislamu, ya Budha, na hizo zote, wamekufa na wamo kaburini. Bali sisi tuna kaburi tupu, na Kristo aliye hai aliye hapa pamoja nasi, usiku wa leo, akijitambulisha Mwenyewe katika Utu wa Roho Mtakatifu, akitenda kazi kupitia kwetu na kuonyesha ya kwamba Yeye Ndiye Neno la wakati huu. Yeye ni Neno, kuzifanya ahadi hizi za wakati huu kuwa hai. Na kama anaweza kufanya ahadi iliyotambulishwa, kujitambulisha Mwenyewe kwayo, ni zaidi sana vipi ataitimiza ahadi Yake ya uponyaji, ambao tumeona ukifanywa miaka hii yote!

²⁸⁸ Iangalie mikono hiyo ya waaminio, Bwana, wakiwekeana. Ninaomba dua hili kwa niaba yao, Bwana, kwamba kila mmoja

wao ataponywa. Tujalie. Jalia nguvu za Yesu Kristo zitapakae ndani ya kila mmoja wao. Na jalia imani ije, kusudi waweze. . . La, jalia hata mtu asijue mtu huyo ni nani, aliyewawekea mikono. Lakini tunajua ya kwamba Wewe upo hapa, nasi tunakugusa kwa imani yetu.

²⁸⁹ Shetani, katika Jina la Yesu Kristo, waache wasikilizaji hawa. Toka ndani ya watu hawa, ili waweze kwenda na kuwa huru, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Vema, ndugu.

²⁹⁰ Ni wangapi wenu ambao sasa wanaamini kwa moyo wenu wote ya kwamba Yesu Kristo anawaponya? Simama kwa miguu yako, useme, “Ninaamini.” Vema, sasa maombi ya imani yameombwa. Ajabu sana. Sawa. Mungu awabariki. Hilo latosha. Amina.

²⁹¹ Sasa, ni wangapi, huku mikono yenu imening’inia chini namna *hii*, ambao hawakumwamini Kristo, wala hujawahi kumpokea kama Mwokozi wako, nawe ungetaka kumwinulia mikono yako? Useme, “Mbele Zako, Bwana, Mungu yeye yule ninayeamini ya kwamba atanihukumu kwenye Siku ya Hukumu, Yeye yupo hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, sasa nitakukubali kama Mwokozi wangu.” Inua mkono wako, useme, “Nitafanya hivyo.” Naam. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe. Mwingine? Wewe. Mungu akubariki. Ajabu. Pale, Mungu akubariki. Mwingine? “Nitainua mikono yangu. Sasa nataka kumkubali wakati akiwa hapa, niko Mbele Zake.”

²⁹² Kamwe hutakuwa karibu zaidi, mpaka utakapomwona uso kwa uso. Kwa sababu, hapa, tabia Zake zote zimetambulishwa hapa sasa, kuwaponya wagonjwa, na kujua siri za moyo. Yeye Ndiye Neno la wakati huu.

²⁹³ Mnaamini hivyo? Inueni mikono yenu sasa, mtu mwingine yeyote. Mwingine yeyote sasa anayetaka kumkubali kama Mwokozi, inueni mikono yenu juu sana sasa, tupate kuiona. Vema. Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Wengine, nakisia, wanane ama kumi, kumi na watano, waliinua.

²⁹⁴ Sasa inamisheni vichwa vyenu sasa hivi, tunapowaombea, kila mmoja. Ikiwa umesimama karibu na wale walioinua mikono yao, Mkristo fulani na awawekee mikono.

Mmoja wa wachungaji na aje hapa, tafadhali, upesi sana.

²⁹⁵ Nitamwomba mmoja wa wachungaji hawa aombe dua kwa ajili yenu sasa, kwa hao watu waliosimama sasa hivi. 

KRISTO AMETAMBULISHWA YEYE YULE KATIKA VIZAZI VYOTE SWA64-0415
(Christ Is Identified The Same In All Generations)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliuhubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 15 Aprili, 1964, kwenye Jumba la Mikutano la McKay huko Tampa, Florida, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org